Tangu Wakati Huo

Asanteni. Tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa ajili ya maombi. Kama kuna haja usiku wa leo, na ijulikane kama mkono ulioinuliwa kwa Mungu kwa ajili ya haja.

2 Baba yetu wa Mbinguni, Wewe unaiona mikono na unajua yaliyo moyoni mwao, unajua kile tunachohitaji, na Wewe umeahidi ya kwamba utakuwa Msaada utakaoonekana tele wakati wa shida, nasi tunaomba ya kwamba Wewe utawakomboa na kila shida. Tujalie, Bwana.

3 Tunakushukuru kwa yale unayofanya nchini leo, kote ulimwenguni ile siri kuu ya Injili inafunuliwa kwa maelfu ya watu tukiamini ya kwamba unaliweka Kanisa tayari ukalipokee katika Kuja Kwako. Ninaomba, Baba, ya kwamba kutakuwa na wengi kutoka kwenye mji huu ambao wataenda katika Unyakuo huo mkuu ambao tunautazamia wakati wowote. Tujalie.

4 Tubariki pamoja sasa, kwa kuwa tumekusanyika katika Jina la Yesu, tukimwomba Mungu, katika Jina Lake, awe pamoja nasi. Tuko mikononi Mwako, Bwana, fanya nasi upendavyo. Amina.

5 Hakika ninayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu tena, usiku wa leo, kusimama hapa pamoja na watu hawa, na kuamini ya kwamba Mungu atatushughulikia tena, usiku wa leo. Neema Yake tele na ikae juu yetu daima. Jambo la ajabu jana jioni, tulipomwona akiwaponya watu njiani; nasi tukatoa usiku huo kwa kuwaombea wagonjwa. Kwa kawaida sisi hujaribu kutochukua muda mwingi sana kwa ajili ya wagonjwa, tunaomba kila usiku, yote yamejumuishwa, jambo kuu tunalojaribu kufanya ni kuwafanya watu waone ya kwamba Kristo hajafa, kwamba Yeye yu hai. Na kama tunaweza tu kumwona Yule aliyetutolea ahadi hizi zote kuu yupo hapa kuthibitisha ahadi hizo.

6 Sasa, mnachoona hapa, mkutanoni, tunapokuwa na siku hizo usiku namna hiyo, kwa kweli, hakuna njia ya kulielezea. Nilikuwa tu nimesimama huko nje wakati dada kadhaa walipokuja, watatu, ninaamini, ndipo dada mmoja akaangalia chini, kasema, "Ndugu Branham, ninataka kumshukuru Mungu kwa ajili ya rehema Zake kwa watoto wangu usiku wa leo, wapendwa." Wakija huku, gari moja lilitokea nao wakapinduka, na kila kitu, lakini kamwe hata hawakukwaruzwa. Wako papa hapa sasa, wameketi kwenye vipandio vya mbele wakijaribu kusikia ujumbe kutoka nje. Neema ya ajabu! Wakati mwingine, tuseme, kama nilivyosema jana usiku (wakitoka Emau), Yeye

hutembea pamoja nasi kila siku, na kutusaidia, na hata hivyo, labda hatulitambui mpaka tu. . . wakati mwingine.

7 Sasa, maono ni kitu cha zaidi ya chochote ambacho mtu yeyote anaweza kuelezea. Ni Mungu asiye na kikomo Ndiye ajuaye mwisho tangu mwanzo, na kutabiri mwisho, na kusema mwisho utakavyokuwa, kwa sababu Yeye alijua kila kitu na angali anajua kila kitu. Hakuna kitu ambacho Yeye hajui. Wala Yeye—Yeye hajui zaidi sasa kuliko alivyojua hapo mwanzo, kwa sababu Yeye hana kikomo. Mnaamini Mungu hana kikomo? Kama sivyo, Yeye si Mungu.

8 Kwa hiyo basi, wazieni tu, hapa kuna ninii tu. . . Huwezi kuchanganua kutokuwa na kikomo. Ni kama tu. . . Kuwa bila kikomo ni kama tu kuwa, kile mimi. . . ningesema, Milele. Milele kamwe haikuanza, kwa hiyo haina mwisho. Mliwahi kuwazia hilo? Na kila kitu, kinachoanza, kina mwisho. Mnaona? Na vitu visivyo na mwisho ni vitu, ambavyo havikuwa na mwanzo.

9 Na hiyo ndiyo sababu hatuna budi kuwa na Uzima wa Milele. Sisi ni sehemu ya Uzima wa Mungu, ambao neno *Milele*, ndugu wakijua ya kwamba ninii. . . linatokana na neno la Kiyunani *Zoe*, ambalo linamaanisha "Uhai wa Mungu Mwenyewe." Hiyo ndiyo sababu tunakuwa watoto Wake Mwenyewe. Mnaona? Ni Uzima wa Milele ndani yetu. Uzima ulio ndani yetu kamwe haukuanza, hauwezi kwisha, hauwezi kufa zaidi ya vile Mungu asivyoweza kufa, kwa sababu ni wa Milele. Kuna Kitu kimoja tu cha Milele, na hicho ni Mungu. Nasi tunakuwa sehemu Yake kwa sababu tunakuwa wana na binti za Mungu. Ni ajabu jinsi gani kujua ya kwamba Mungu ameahidi!

10 Tunahitaji tu muda zaidi katika miamsho. Siku moja natumaini kupata hema ambalo nimekuwa nikitaka kupata kwa muda mrefu sana, nami. . . na kwa hiyo tunaweza kukaa muda mrefu zaidi kidogo, ili tuweze kuondoa hisia zote za kigeni. Watu hawataki kuwa hivyo, lakini kwa kweli wako hivyo tu. Mnaona? Tuko hivyo. Tunakusanyika pamoja kama kundi la watu kokote tu tunakotoka, madhehebu mbalimbali yanatushika, chochote kile.

11 Ndipo, tunapoingia katika makusanyiko kama haya, ndipo mnaona jambo la ajabu likitukia, kwa namna fulani linatushtusha kabisa, na kwa hiyo linaninii. . . hasa sana kwa wahudumu, si kwa hawa, bali kwa wahudumu, zaidi sana. Wao ni wachungaji, wanawalinda kondoo wao, mnaona, na kwa hiyo wanaangalia kila kitu kidogo. Huninii. . . huwezi kumlaumu huyo mtu, unaona, kwa sababu hana budi kuelewa kwanza.

12 Lakini hilo jambo, kama mtu akikosoa vikali na kulikataa, basi kuna kasoro hapo, kama mtu hatatilia maanani ku—kulichunguza kote katika Biblia na kulitafuta. Angalieni, hivyo ndivyo Mafarisayo walivyomtendea Bwana wetu.

13 Hivi mlijua kila nabii, aliyewahi kuinuka duniani, kamwe hakupokelewa na watu? Kila mjumbe Mungu aliyewahi kumtuma hakupokelewa, wala hawakujua huyo mjumbe alikuwa ni nani mpaka alipokuwa amekufa na kuondoka. Sasa, hiyo ni kweli.

14 Ninyi Wakatoliki hapa, jinsi mlivyokosa kumjua Joan wa Arc! Wengi wenu watoto wa shule mnakumbuka hilo. Mwanamke huyo alikuwa ni mwanamke wa Mungu, alitabiri, alikuwa ni mwanamke wa kiroho. Mnajua vile kanisa lenu lilifanya? Lilimchoma moto kama mchawi. Hiyo ni kweli. Bila shaka, miaka mia mbili baadaye mlifanya toba, mkaichimbua miili ya makasisi hao na kuitupa mtoni mlipotambua alikuwa ni mtakatifu. Mnaona? Siku zote ni yaliyopita.

15 Kamwe hawakumjua Patrick. Nao watu wanafikiri ati Mtakatifu Patrick alikuwa Mkatoliki? Kadiri nilivyo mimi. Angalieni mahali shule zake ziliko huko Ayalandi, hana misalaba na misalaba yenye sanamu kwake, alimshutumu papa vikali. Lakini bila shaka, wao wanajaribu kumfanya wa kanisa, lakini ni uongo.

16 Mimi ninatoka katika familia ya Kikatoliki, ninajua ninalozungumzia, pia nina *Kweli Za Imani Yetu,* na vitabu hivyo vyote ambavyo nimevisoma, kadiri uwezavyo kusoma. Na kwa hiyo . . . Lakini mambo hayo, mnaona, wanayapita. Hawakumjua Eliya kamwe, kamwe hawakumjua Yohana, hawakumjua Yesu mpaka baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka. Na sasa, Roho Mtakatifu anashuka, nao hawatamjua, kama tu katika siku za Nuhu, mpaka gharika ije na kuwaondoa, hiyo ni kweli, gharika kuu iingie.

17 Lakini kama hao Mafarisayo wangeketi tu chini, na kuwaza! Yesu aliwaambia, "Mliwapiga mawe manabii. M—mlizipaka chokaa ninii zao—kuta zao za ninii zao . . . mliyapaka chokaa makaburi yao, nanyi ndinyi mliowaweka mle." Mnaona? Kasema, "Vipi . . .? Ni yupi kati ya manabii aliyetumwa na Mungu ambaye baba zenu hawakumpiga mawe?" Mnaona? Na hao . . . kadhalika. Inatubidi kuketi chini na kuyatafakari.

18 Kulikuwako na hao, kidogo kama Nikodemo, yule mwaminio wa siri, aliyekuja usiku, akaingia kisiri, kasema, "Rabi, tunajua Wewe ni Mwalimu uliyetoka kwa Mungu, hakuna mtu angeweza kufanya mambo ufanyayo Wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye."

19 Mwangalie maskini Yairo, huenda alijifanya kama kwamba hakuamini katika uponyaji wa Kiungu, mpaka binti yake mdogo akawa amelala mahututi. Mungu anayo njia ya kuvuta hilo na kukufanya uonyeshe jinsi ulivyo hasa. Unaona? Ndipo ikadhihirika wazi, yeye alikuwa ni mwaminio; na ilibidi tu ifikie mahali fulani kumfanya alione. Mungu ni mwema sana kwetu, nasi tunashukuru kwa ajili ya wanaume na wanawake, kama

walioketi hapa usiku wa leo, wanaoamini Injili, wanaoamini katika uponyaji wa Kiungu, wakiangalia.

20 Sikuzote nimesema kuhusu madhehebu yetu, ninayaamini, nami ninaamini ya kwamba ni mazuri, yanatumikia kusudi fulani, lakini mnaona, tunapounda dhehebu, asilimia tisini yetu tunapoliunda moja, tunaandika, "*Hili* ndilo tunaloamini, *hamna lingine*." Kama mngesema, "*Hili* ndilo tunaloamini *koma*, pamoja na kadiri Mungu atakavyotuongezea," hilo ni sawa basi. Hilo—hilo ni sawa. Mnaona? Hilo ni kweli kabisa.

21 Wakati Nguzo ya Moto ilipoondoka, Israeli iliambatana Nayo. Na katika Agano Jipya, wakati ilipoanza kuondoka, kama tu vile hasa ilivyofanya katika Agano la Kale, waliondoka vivyo hivyo, ilibidi Israeli waifuate hiyo Nguzo ya Moto, na kupiga hema chini Yake, kisha wakati ilipoanza kuondoka katika huu wa mwisho, kwenye yale matengenezo, Martin Luther aliiona.

22 Ndipo basi, mara Luther alipoondoka, waliundia dhehebu kazi ya Luther, Mungu akaondoka moja kwa moja chini yake, naye Wesley akaiona, naye huyo akaondoka. Baada ya Wesley, na—na Asbury, na wengi wa hao wengine, wakati . . . baada ya wakati wao, ndipo nini kilitukia? Wakaunda dhehebu chini Yake, Mungu akaondoka moja kwa moja kutoka chini yake, akaendelea mbele moja kwa moja. Mnaona?

23 Na sasa, sisi Wapentekoste tunafanya jambo lile lile. Huwezi kumwundia dhehebu Roho Mtakatifu, huwezi kufanya hivyo. Tunaamini katika madhehebu kudumisha udugu na kadhalika, hutimiza kusudi jema, lakini sikuzote inyoshe blanketi kumfunika huyo ndugu mwingine, mnaona, na kuuweka moyo wako wazi upate kile ambacho Mungu yuko tayari kutuma juu yetu. Hiyo ndiyo njia ya kufanya hivyo, huo ni udugu halisi, na kwa hiyo ninapenda hilo. Wakati sisi . . . Kama ningeweza kuona wakati ambapo kanisa la Kipentekoste . . .

24 Sasa, Pentekoste si dhehebu, Pentekoste ni Tukio. Ninajua takriban Walutheri wengi na Wabaptisti na Wapresbiteri waliopata Tukio la Kipentekoste kama Wapentekoste wanaojiita Wapentekoste. Kwa hiyo Pentekoste ni Tu—Tukio.

Wakati fulani uliopita . . . Nitaanzia hapo, kisha ningeuacha ujumbe wangu, ama . . . Nipeni tu wakati wa kusema hivi. Sivyo? Nivumilieni, ni vema.

25 Nilikuwa Minneapolis, Minnesota, hiyo ni nchi kuu ya Norwe, nami nilikuwa na mkutano, nasi tulikuwa kwenye jengo fulani kuu, nami nilikuwa huko moja kwa moja kwenye majira ya baridi kali, ama, majira ya kuchipua. Nami nilikaa kwenye hoteli ndogo ya bei rahisi huko chini . . . Ninaamini ya kwamba Wakristo hawapaswi kuwa tu na kila kitu cha kifahari sana. Yesu hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake, mnaona, nasi tunajaribu kuwa na yaliyo bora kuliko yote, na usalama *mwingi sana* na kadhalika. Aibu kwetu. Mnaona?

26 Lakini hoteli ndogo, na hiyo. . . Usiku mmoja nilipoingia kutoka kanisani, kesho yake asubuhi nilitoka, nikapata kiamshakinywa, ndipo niliporudi kulikuwako na ba—barua ya kurasa ishirini na mbili kwenye shubaka kwa ajili yangu. Jinsi mtu huyo alivyopata kujua nilikuwa kule, sijui. Kwa hiyo nikaisoma, na loo, nena kuhusu ukosoaji mzuri, ulikuwa mzuri. Nami ninauthamini huo, hakika ninauthamini. Mtu yeyote ambaye kweli ana jambo fulani, na anataka kukosoa, hilo hutusahihisha. Mnajua, ukosoaji hutoa bidhaa nzuri, unaona, wakati tukiwa tayari kuupokea, kuujaribu.

27 Kwa hiyo mtu huyu alikuwa amenikemea vibaya sana. Alikuwa mshauri wa chuo fulani, naye akasema, "Ulikuwa ukizungumza jana usiku kuhusu kuwa katika huduma miaka ishirini na mitano," ni thelathini na mmoja sasa, lakini akasema, "miaka ishirini na mitano," kasema, "nilikuwa katika huduma kabla hujazaliwa." Naye akasema, "Na baadhi. . . Nimeona mambo ya ajabu sana." Kisha kasema, "Niliendesha gari jana usiku, maili kumi na tano kwenye dhoruba mbaya ya theluji inayopofusha, nilifikiri ningemwona mtumishi wa Kristo. Nami nilipata nini? Ila mpiga ramli hodari sana."

28 Kisha akasema. . . Wala asingeniita "Ndugu," alisema tu, "Branham," kwa hiyo, hilo lilikuwa ni sawa. Kwa hiyo akasema, "Na wazo lenyewe. . . Hiyo theolojia, ndiyo iliyooza kuliko zote niliyowahi kusikia maishani mwangu," halafu kasema, "kwa mfano, ulisema hivi, kwamba Shetani asingeweza kuponya." Kasema, "Mtu anayesimama mbele ya watu wengi sana kama unavyofanya na kufanya kosa kama hilo," kasema, "mbona, ni mbaya sana."

29 Akasema, "Sasa, hebu nikwambie jambo fulani, kijana," akasema, "huku nyuma ya seminari yetu hapa, ama mahali petu," kasema, "kuna mwanamke aliye na roho ya uchawi." Kisha kasema, "Amevaa aproni kubwa," tena kasema, "watu huja pale kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu." Kisha kasema, "Wao. . . Naye anaenda, na kuwapapasa kila mahali, namna *hiyo* kwa mikono yake," kisha kasema, "ndipo muda si muda wajua, wanatia pesa kwenye aproni hii."

30 Sasa, mngeweza kuona papo hapo, linakiuka Maandiko, na kwanza kabisa si sahihi, mtu yeyote aliye na maarifa yo—yoyote ya Mungu. Mnaona? Kisha kasema, "Kisha anang'oa nywele kidogo kutoka nyuma ya shingo yake, akatoa damu kutoka kwenye mishipa yao, na kuzipaka nywele hizi, anashuka kwenye kijito kidogo nyuma ya mahali hapo, anazitupa juu ya kichwa chake hadi kwenye hicho kijito."

31 Tena kasema, "Kisha anaanza kuwaendea watu, na kama akilazimika kuangalia nyuma," kasema, "hao watu. . . huo ugonjwa unawarudia hao watu; asipofanya hivyo," kasema, "basi, mbona, huo ugonjwa haurudi."

32 Kisha kasema, "Tumechunguza jambo hilo," halafu kasema, "asilimia *fulani* yao wanapona." Ndipo kasema, "Wazo lenyewe la wewe kusema ati Shetani asingeweza kuponya!" Vema, akaendelea na mambo chungu nzima.

33 Nami nikawazia, "Vema, kama alichukua muda wa kutosha kuniandikia kurasa ishirini na mbili, ninapaswa kumwandikia angalau kurasa mbili tena kama jibu." Kwa hiyo nikakaa chini vizuri nilivyoweza, hata siwezi kabisa kusoma mwandiko wangu mwenyewe, nami nikamwandikia ovyoovyo kitu fulani kidogo. Nikasema, "Ndugu mpendwa," ilinibidi kumwita hivyo, mtu yeyote ambaye amekuwa akihubiri kwa miaka hamsini anapaswa kuchukuliwa kama "Ndugu," kuihubiri Injili, haidhuru imekuwaje. Nami na—na—namchukua kama ndugu yangu.

34 Basi nikasema, "Hakika ninathamini na kuiheshimu sana, miaka yako mingi ya huduma kwa ajili ya Bwana wetu." Kisha nikasema, "Bi—bila shaka ninamshukuru Mungu, kukujalia uishi kwenye umri huu mzuri wa uzeeni, na mambo ambayo umefanya," na kadhalika. Basi kulikuwa na ndugu mwingine pamoja naye, kwa hiyo basi . . . wa chuo hiki.

35 Ndipo muda si muda mwajua, ni—nikasema, "Lakini ninii . . . Ni jambo geni sana kwangu," nikasema, "kwamba unanikosoa sana kwa kusema ya kwamba Shetani asingeweza kuponya." Nikasema, "Sasa, ulisema Shetani angeweza kuponya, Yesu alisema, 'Kama Shetani anaweza kumtoa Shetani, basi ufalme wake umegawanyika.'" Nikasema, "Sasa, nitamwamini nani? Wewe, ama kile Kristo alichosema? Shetani hawezi kuponya, Kristo alisema hivyo. Anajipinga mwenyewe, hawezi kuponya."

36 Lakini nikasema, "Na kujaribu kuelezea, kama mtanisa- . . . kunradhi," nikasema, "kwa mshauri wa chuo, ama mtu mashuhuri kama wewe, kwamba ningetaka kukwambia, nikiwa mmishenari, nimeona watu wakija kwa sanamu na kuponywa. La Salle, Lorraine, Ufaransa, kuna sanamu ya mwanamke; na huko chini Paris niliona ambapo walikuwa na mwa—mwanamke, mwanamke aliyekufa kule, nao walikuwa wamesugua na kutoa jiwe zima nyuma yake kuzuia janga lisiingie mjini. Nimeona mambo hayo yote.

37 "Nami nimewaona watu Marekani, wanaojiita waponyaji wa Kiungu, na kusema, 'Nina uponyaji *hapa*, na uponyaji *huku*, na uponyaji katika *hiki*.'" Nikasema, "Ni jambo lile lile." Unaona? "Uponyaji uko katika Kristo." Kweli kabisa.

38 Lakini nikasema, "Watu . . . Sina shaka, kwamba watu hao walipona. Lakini hili hapa linalotukia, ninii . . . uponyaji wa Kiungu umewekewa msingi juu ya . . . juu ya imani. Na hao watu wakimjia huyo mchawi unayenena habari zake, bila shaka walifanya hivyo, wanafikiri wanamkaribia Mungu kupitia

kwa mchawi huyo, na juu ya msingi wa imani yao Mungu huwaponya." Mnaona? Wao—wao . . . Hakika. Wewe . . . Kama una imani ya kutosha kuliamini, litatukia. Hiyo ni kweli kabisa.

39 Lakini nikasema, "Jambo la ajabu kwangu, kwamba mshauri wa chuo cha Kilutheri angewekea msingi imani yake juu ya ujuzi fulani badala ya Neno la Mungu wakati Kristo alisema ya kwamba Shetani asingeweza kuponya. Ni majilio yao, wakiamini wanamjia Mungu kupitia kwa mchawi, na kupitia kwa sanamu, na kadhalika. Ni watu wasio na hatia wanaoamini ya kwamba Mungu huponya."

40 Vema, yapata mwaka mmoja baadaye nilikuwa nimerudi huko kwa ajili ya Wafanyabiashara Wakristo mkutanoni. Ndipo ndugu mwingine wa thamani, Dk. Hegre wa Chuo cha Bethany, akaniandikia barua, na kusema angependa niende kule. Niliogopa kwenda, maana niliwajua hao mabingwa wa kielimu. Nilikuwa na . . . Maskini elimu yangu ya shule ya msingi isingeweza kustahimili yao. Basi akanialika, nami nikamwambia Ndugu Moore, "Kama utaambatana nami sasa na yapite elimu yangu, nitakugonga goti na langu nawe uchukue mamlaka kutoka hapo," na kwa hiyo akakubali kwenda.

41 Kwa hiyo tukaketi mezani, wakatuwekea meza nzuri huko chini kwenye ukumbi wa mazoezi. Maskini wanawake wazuri wa Kilutheri waliandaa chakula chetu kizuri cha jioni, kizuri sana. Basi wa- . . . Dk. Hegre aliketi karibu nami, naye akasema, "Sasa, Bw. Branham," tulipomaliza, akasema, "Ninataka kusema jambo hili moja, naomba msamaha," yale huyo mtu aliyosema. Kasema, "Sasa, lakini mimi . . . "

Nikasema, "Hilo lilisamehewa hapo mwanzo."

42 Naye akasema, "Tuna njaa, hapa Bethania." Kasema, "Sisi ni . . . " Kuna ninii kuu . . . Wanafunzi, kama hawawezi kujilipia karo, wana mamia ya ekari za mahindi na kadhalika wanayolima, na kujilipia kote chuoni, shule nzuri sana. Naye akasema, "Tuna njaa. Tunasoma habari za Mungu." Kisha kasema, "Tulipata *mle* ndani, miaka kadhaa iliyopita, kuhusu Roho Mtakatifu na jinsi alivyotenda kazi."

43 Kisha kasema, "Tukawaendea Wapentekoste waliodai kuwa Naye." Pia kasema, "Tumewaona wakipiga teke viti, wakivunja madirisha, na kadhalika." Akasema, "Wana nini?"

Nikasema, "Roho Mtakatifu."

Basi akasema, "Huyo?"

44 Nikasema, "Hakika. Wana mvuke mwingi sana inawabidi kuupuliza utoke kwa filimbi, hawatauweka kazini, waache ukatende kazi," Nikasema, "ni hivyo tu. Kuna mvuke mwingi sana unaopulizwa . . . unaongezeka, inawabidi kuutoa kwa njia fulani." Nami nikasema, "Wao wananinii tu . . . Kama mngeweka nguvu zizo hizo, kitu hicho hicho kazini, katika imani, kwa

Neno la Mungu, na kuanza kukiendeleza, mnaona, badala ya kukipulizia tu. Mnaona? Ni. . .Roho Mtakatifu huuongezea mle ndani."

Naye akasema, "Vema, basi unafikiri sisi Walutheri tuna nini?"

45 Nikasema, "Roho Mtakatifu." Ndipo akanyamaza na kuniangalia, nami nikawaza, "Bwana, kama uliwahi kunisaidia, nisaidie sasa, maana hakika nimejitia. . . "

Akasema, "Vema. . . "

Nikawazia, "Laiti ungenisaidia tu, Bwana." Daima amefanya hivyo, miongoni mwa wachawi na pepo, na kote ulimwenguni katika mahali pagumu.

Naye akasema. . .Nikasema, "Vema, sikiliza, Bwana."

46 Akasema, "Tulienda. . .tukaruka kwa ndege hadi Los Angeles kwa mtu aliyeandika kitabu juu ya karama zote." Kisha kasema, "Tulipofika kule, alisema, 'Mimi sininii. . .Sina yoyote ya hizo.' Kasema, 'Ni—niliandika tu habari zake.'"

47 Akasema, "Vema, tungeweza kufanya jambo lile lile hapa, maana alilichukua moja kwa moja kutoka kwenye Maandiko; tunataka kuiona. Usiku huo tuliposhuka kule na kuona jambo hilo, tulikuwa tayari tumeamua ilikuwa uongo, na hiyo ndiyo sababu tulikuita mpiga ramli hodari."

Nikasema, "Vema, ninakusamehe hilo kama nilivyosema." Lakini nikasema. . .

Akasema, "Tu—tuna nini sisi Walutheri?"

48 Nikasema, "Nilisema, 'Roho Mtakatifu.' Sasa sikilizeni," nilifikiri ningeweka. . .kuzungumza kwa njia yake mwenyewe apate kujua, nikasema, "wakati mmoja mtu aliandaa shamba kubwa, naye akapanda zao la mahindi. Aliendelea kuliangalia siku baada ya siku, mpaka asubuhi moja akatoka, na kulikuwa na majani mawili madogo yakikua." Mnajua jinsi mahindi yalivyo yanapochipuka. Nikasema, "Huyo mtu alisimama barazani mwake na kusema, 'Mungu asifiwe kwa ajili ya zao la mahindi.'" Nikasema, "Sasa, je, alikuwa nalo?"

Kasema, "Vema, alikuwa na mwanzo wake."

49 Nikasema, "Basi, tungesema, 'Kwa uwezekano alikuwa nalo.' Punde si punde hao. . .Hao walikuwa ni ninyi Walutheri hapo mwanzo." Nami nikasema, "Punde si punde majani hayo yakakua, kisha kishada kikatokea, hicho kilikuwa ni Wamethodisti."

50 Nami nikasema, "Ndipo Wamethodisti wakawageukia Walutheri na kusema, 'Sina haja nanyi, mimi ni kishada, hamumo ndani yake.' Lakini mnaona, ilibidi litumie hilo jani tena kwa sababu. . .ili chavua iangukie humo, ndipo suke lichipuke, Pentekoste, pamoja na ya asili, kama ilivyokuwa

hapo mwanzo, punje iliyoingia ardhini, ilikuwa inazaa punje." Nikasema, "Sasa, tuna kuvu nyingi sana kwenye suke, lakini tuna punje pia." Hiyo ni kweli. Nikasema, "Kama ilivyokuwa hapo mwanzo."

51 Nikasema, "Hiyo ndiyo sababu niko miongoni mwa watu, wao ni watu wa Mungu." Nami nikasema, "Mnaona, kanisa la Kipentekoste ni kanisa la Kilutheri lililoendelea mbele, kwa sababu uhai ule ule uliokuwa kwenye jani ulifanya mahindi." Hiyo ni kweli. Naye akalipata.

52 Akarudisha sahani yake upesi na kusimama. Akasema... akawaangalia wenzake, wanafunzi wote, na kadhalika, na washauri, na lile kundi, naye akasema, "Sisi hapa Bethania tuna njaa ya Roho Mtakatifu." Kasema, "Ndugu Branham, tufanye nini tupate kumpokea?"

Nikasema, "Geuzeni uso wenu kutoka mezani, mwende muuegemee ukuta, na kupiga magoti kuelekea ukutani, na muwe waaminifu kabisa."

53 Nikashuka na kuwawekea mikono, arobaini na kitu wakampokea Roho Mtakatifu papo hapo, na sasa wana zaidi ya mia nne katika shule hiyo wakifanya ishara za kila namna, miujiza. Ni kitu gani? Hiyo ni Pentekoste ya Kilutheri. Mnaona? Kila mahali, kila mahali Roho Mtakatifu...Hatuwezi kulifungia Hili chini na kusema, "Sisi Wapentekoste tunalo." Mungu amevunja mpaka huo na kuingia mle ndani, na kuchukua kila kitu kilichokuwako, "Kwa yeyote atakaye, na aje." Mnaona? Ni kwa ajili ya watu.

54 Pentekoste ni Tukio. Katoliki ya Kirumi, Othodoksi ya Kiyahudi, chochote walicho, Mchina, Mbuddha, loo, kila kitu, Injili ni kwa ajili ya yeyote atakaye, anaweza kuja.

55 Loo, ninalipenda tu, na kulipenda tu. Loo, jinsi ninavyolipenda! Nami ninajua ya kwamba Mungu anaweza, katika siku ya mwisho, kuinua wale ambao amesema ya kwamba angewainua, ninaamini hilo. Ninaamini katika ufufuo wa kiama, ya kwamba wale waliokufa huko nyuma katika imani ya Kilutheri hapo mwanzo hawataninii...hawa... hawatawatangulia hawa..."Parapanda ya Mungu italia, na wote waliokufa katika Kristo watafufuka." Hiyo ni kweli.

56 Ninaamini Kanisa linafikia uka-...Ukamilifu wake daima, ukija. Na wakati adui anapokuja kama mafuriko, Roho wa Mungu anainua kiwango dhidi yake, kubwa zaidi, na kubwa zaidi, kujengeka zaidi. Sasa, ni moja kwa moja kwenye jambo hilo la mwisho, yale niliyokuwa nikizungumzia jana usiku. Loo, ninaamini ya kwamba Yeye atakuja. Nami ninaamini ya kwamba maskini hii miili yetu dhaifu itabadilishwa na kufanywa kama Mwili Wake Mwenyewe mtukufu.

57 Huku nikihubiri jinsi alivyowageuza Ibrahimu na Sara, huko nyuma, kuwa kijana mwanamume na mwanamke wapate mtoto

huyo, nikisema ya kwamba, wakati fulani uliopita nilikuwa nikizichana nywele hizi mbili ama tatu nilizobaki nazo. Mke wangu akaniambia, akasema, "Billy, karibu una upara."

Nikasema, "Ila sijapoteza hata mmoja wazo."

Akasema, "Basi, naomba uniambie mahali zilipo."

58 Nikasema, "Mpenzi, niambie zilikokuwa kabla sijazipata, popote pale zilipokuwa wakati huo, zimerudi huko sasa zikiningojea niziendee." Amina. Hiyo ni kweli. Hiyo ni . . . "Hata nywele za kichwa chako zimehesabiwa. Hakuna hata mmoja utakaoangamia." Hiyo ni kweli kabisa. Tumeumbwa kutokana na nini? Tumeumbwa kutokana na elementi kumi na sita, hizo ni potashi, na petroli, na nurulimwengu, na kadhalika. Na hizo ndizo hasa Mungu alizo nazo hivi . . .

59 Yeye ni Mkandarasi mkuu. Kabla hajapata kuwa na mwanadamu duniani, aliweka nyenzo, kama mkandarasi anayejenga sehemu ndogo. Alikuwa anataka kumfanya mtu kwa mfano Wake Mwenyewe na kuwapa dunia wakae, nao walikuwa miungu wadogo kuliko Yeye alivyokuwa.

60 Yesu alisema, "Torati yenu inasema ninyi ni miungu." Hiyo . . . Mamlaka, wafalme, mamlaka juu ya nchi, angeweza kufanya lolote alilotaka. Ndipo dhambi ikaingia, na sasa mwanamke anazaa mtoto, na anapozaa, mtoto huyo hana budi kufa. Mnaona? Ni kweli kabisa, ni kuzaliwa kulikopotoshwa. Lakini basi wakati kuzaliwa upya kunapoingia, kunasahihisha uzazi huo uliopotoshwa na kukupa Uzima wa Milele kupitia kwa Baba, Yesu Kristo.

61 Loo, ndugu! Yesu alisema, "Yeye alisikiaye Neno Langu . . . Yeye aulaye mwili Wangu, na kuinywa Damu Yangu, yuna Uzima wa Milele; nami nitamfufua tena katika siku ya mwisho." Amina. "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu," wala hakuna kilichopotea. Amina. Yeye atawafufua tena katika siku ya mwisho. Mauti wala chochote kile hakiwezi kututenganisha, daima tuko katika Uwepo wa Mungu. Jinsi ninavyopenda hilo!

62 Nukuu ndogo . . . ni kwa nadra sana mimi . . . Sisemi mengi sana, mimi huzungumza tu sana, wala sisemi chochote. Lakini wakati mwingine . . . Mimi si kama ndugu wahubiri hapa, ambao ni wasomi na wanajua jinsi ya kuweka mambo hayo katika utaratibu. Lakini wakati mwingine mimi husema jambo fulani, nalo hu—hunisaidia sana, hata hivyo. Na si muda mrefu uliopita nilisema jambo ambalo lilikuwa muhimu sana kwangu.

63 Nilikuwa nikiwazia juu ya hakikisho la kuvuka kwetu. Halafu basi . . . Tunaona ya kwamba wakati mmoja watoto wa Mungu walikuwa watumwa huko chini Misri. Waliwatupia mkate, ulioshika kuvu, uliooza, chochote kile, iliwabidi kuula. Waliwabaka wasichana wao, wakawaua wana wao, chochote wangeninii . . . Nao walikuwa ni watu wa Mungu. Hiyo ni kweli.

Sasa, na kwa hiyo walikuwa ni watumwa, wala wasingeweza kujizuia.

64 Lakini siku moja, akishuka kutoka nyikani, akaja nabii pamoja na—na Nguzo ya Moto juu yake, naye akawaambia Neno la Mungu, ya kwamba kulikuwako na nchi iliyojaa maziwa na asali ambayo Mungu alikuwa amemwahidi Ibrahimu angewapeleka watoto wake. Naye nabii huyu alithibitishwa kuwa wa Mungu kwa ishara na maajabu aliyofanya alipokuwa Misri, nao watu wakamwamini mtu huyu.

65 Naye akatoka Misri, wana wa Israeli walitoka, wakafika mahali pa Kadesh-barnea, ambapo msomi yeyote anajua, ya kwamba Kadeshi-barnea, wakati mmoja, ilikuwa ndiyo kiti cha hukumu cha ulimwengu. Hapo ndipo Israeli ilipokutana na hukumu yake, wakati waliposhindwa kuamini ishara kwamba walikuwa wameleta zabibu na kadhalika kutoka humo nchini.

66 Sasa, kumbukeni, hakuna mtu aliyewahi kuwa katika nchi hii, katika kundi lao, walikuwa wamesikia habari zake. Imani chanzo chake ni kusikia, naye Mungu alitoa ahadi. Mnalipata? Mungu alitoa ahadi, na huyu hapa Musa anakuja, yule nabii mtoro, mle ndani akiwa na ishara zilizothibitishwa, na kuthibitisha ya kwamba ilikuwa ni Mungu akiwapeleka kwenye nchi hii ambayo kamwe hawakuiona. Ni mfano mkamilifu jinsi gani wa siku hizi! Hakuna hata mmoja wetu aliyewahi kuwa huko.

67 Angalieni, walipofika Kadeshi-barnea, kile kiti cha hukumu, walikuwa na shujaa mkuu miongoni mwao aliyeitwa Yoshua, ambalo linamaanisha "Yehova-Mwokozi," *Yoshua*. Sasa, alivuka Yordani akaingia katika nchi hiyo ya ahadi, kisha akarudi na ushahidi kwamba ilikuwa ni nchi nzuri. Alikuwa na zabibu, watu wawili walibeba hilo shada. Wangeweza kuonja mambo ya mbinguni kutoka huko kwenye nchi ya ahadi, nchi nzuri iliyojaa maziwa na asali. Walirudi kuthibitisha ya kwamba hiyo nchi ilikuwa ni kweli, ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa jinsi hasa Musa alivyokuwa amesema lilikuwa kwa uvuvio wa Mungu. Ilikuwako.

68 Wangeweza kuwa na makazi yao wenyewe. Wakaaji . . . Bila shaka, iliwabidi kupigania kila inchi ya barabara waliyopitia. Mungu alimwambia Yoshua katika Yoshua 1, ya kwamba "Kila mahali nyayo za miguu yenu zitakapokanyaga, hiyo ni milki." Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, kila mahali nyayo za miguu yetu zinapokanyaga, ni milki. Endelea tu kutembea, alama za miguu zinamaanisha milki; ichukue tu.

69 Sasa, kumbukeni, ilibidi wapiganie kila inchi ya njia. Baadhi ya watu wanaweza tu kuchukua Upanga wenye mikono miwili na kupigana na kivuli kidogo tu, wengine wanaweza kukata wakaingia kwenye uponyaji wa Kiungu, kila ahadi ya Mungu pamoja Nao. Hiyo ni kweli. Neno ni Upanga, na inahitaji

imani kuutumia Upanga huo, hiyo ni kweli, imani katika Neno lililoahidiwa.

70 Sasa, tunaona ya kwamba wakati. . .Walirudi, nao wakasema wangeweza kuwa na makazi yao na kadhalika. Israeli walivuka wakaingia kwenye nchi ya ahadi, wakajenga makazi, wakawalea watoto wao, wakaishi kwa amani, mataifa mengine yote yaliwaheshimu. Ni jambo zuri jinsi gani! Lakini hatimaye, makaburi yakatapakaa ubavuni mwa vilima. Wakazeeka, wakafa, wakazikwa.

71 Ndipo siku moja akaja Shujaa mwingine mkuu, aliye mkuu kuliko wote: Imanueli. Akashuka, Naye akasema, "Hii siyo ile nchi. Lakini katika Nyumba ya Baba Yangu mna makao mengi, kama sivyo ningaliwaambia. Nami nitaenda na kuwaandalia mahali, kisha nitarudi tena kuwapokea Kwangu."

72 Angalieni, Yeye alikuja kwenye Kadeshi-barnea Yake, Kalvari, ambako alistahimili Hukumu ya dhambi kwa ajili yetu sote. Adhabu ya Hukumu ya Mungu ilitimizwa kwa haki wakati Kristo alipokufa pale Kalvari, akilipa gharama ya dhambi kwa ajili yetu sote. Naye akauvuka Yordani, kama tujuavyo, Yordani ya mauti, akaingia nchini, kisha akarudi siku ya tatu, kama Yoshua alivyofanya, akileta ushuhuda ya kwamba mtu akifa anaweza kuishi tena. Kuna uhai ng'ambo ya mauti, Yeye alilithibitisha.

73 Na sasa, Yeye alisema, "Kwa ajili ya arabuni ya hii, ya kwanza. . ." mnajua *arabuni* ya chochote ni nini, malipo ya kwanza, "enedeni kule kwenye mji wa Yerusalemu mkangoje. Nitawatumia arabuni ya wokovu wenu." Amina. Sasa, ninaanza kujisikia wa kidini. Nao wakangojea mpaka wakapokea arabuni.

74 Sasa, hata wa leo, Roho Mtakatifu yeye yule, ambaye ametuinua kutoka kwenye maisha ya dhambi ambamo tuliishi wakati mmoja. . .Nasi tayari tumekufa katika Kristo, tumezikwa, na kufufuka pamoja Naye katika kufufuka Kwake, na tumeketi sasa katika mahali pa Mbinguni pamoja Naye, amina, tukimwangalia Yeye akitenda kazi miongoni mwetu. Kwa nini? Kwa nini mimi siko huko nje miongoni mwa madhehebu? Kwa sababu ni wale waliokufa na kuzikwa ndani Yake, na kufufuka pamoja Naye katika kufufuka Kwake, na sasa, si tutakuwa, sasa tuko mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, tukiangalia nyuma mahali tulipotoka wakati mmoja; ushahidi wa moja kwa moja kwamba tulipokea sehemu yake kwa sababu tumekufa, na maisha yetu yamefichwa katika Mungu kwa njia ya Kristo, na tayari tumefufuka tena katika ufufuo pamoja Naye. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Amina. Loo, jamani!

75 Kama vile maskini dada mmoja mweusi alivyosema, kunradhi, rafiki zangu weusi, nitaliweka jinsi alivyoliweka,

alikuwa mkusini sana, akasema, "Vema, mimi taka kutoa ushuhuda, usiku wa leo, Daktari."

"Vema. Endelea, Dada."

76 Anasema, "Ninataka kusema hivi: mimi haiko jinsi ninavyopaswa kuwa," kisha akasema, "Mimi haiko jinsi ninavyotaka kuwa, lakini kuna jambo moja la hakika, mimi haiko jinsi nilivyokuwa." Naam, bwana. Alijua ya kwamba alikuwa ameinuka mahali fulani. Amina.

77 Ni kitu gani? Ushahidi kwamba sasa tumekufa, maisha yetu yamefichwa katika Mungu kwa njia ya Kristo, yakatiwa muhuri na Roho Mtakatifu, na kufufuka pamoja Naye, na kuketi mahali pa Mbinguni tukimtazama Yeye. Wazia jambo hilo. Hatuna nguvu, bali mamlaka, hatuna nguvu, tuna mamlaka. Kristo yuna nguvu, Yeye ndiye nguvu, bali sisi tuna mamlaka.

78 Si lazima kuwa mkubwa sana. Hebu mchukue maskini polisi, anayesimama hapa nje barabarani, huku bastola yake imewekwa chini ya ubavu wake, ameegemea upande mmoja, ko—kofia yake imeinamishwa, akivuta masikio yake, huku magari yakishuka kwenda barabarani, yakienda kasi maili sitini kwa saa, hana uwezo wa kusimamisha moja la hayo. La, bwana. Mbona, baadhi yao nguvu farasi mia tatu ama mia nne, yakivurumisha kule.

79 Lakini acha tu atoke huko nje, nyota hiyo ikiangaza, ainue hiyo glavu, filimbi. Unasikia breki zikilia na kadhalika. Yeye hana nguvu, bali ana mamlaka. Amina. Haleluya! Hapo ndipo Kanisa lilipo usiku wa leo. Lina mamlaka kwa sababu limefufuka katika Kristo. Mamlaka!

80 Sasa, kama huyo askari akisema, "Ninaogopa kutoka huko nje. Sijui, huenda ofisi yangu isiniunge mkono," yataendelea kuvumisha. Nami nawaambia, hata mauti yenyewe hupiga breki wakati mamlaka hayo yanapoinuka katika Jina la Bwana Yesu, "Kwa Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; watashika nyoka au kunywa vitu vya kufisha; mtaweka mikono yenu juu ya wagonjwa, nao watapata afya."

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

81 Baba Mungu, tunatoa shuhuda hizi ili tu kuwasaidia watu. Sasa, tuliza nia zetu, Bwana, tunapolikaribia Neno Lako. Jalia, Bwana, kwamba Roho Mtakatifu atachukua maneno machache yafuatayo sasa, na kuyazamisha mioyoni mwa watu, na huenda kengele za furaha za Mbinguni zikalia katika kila moyo. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

82 Katika Injili ya Mathayo Mtakatifu mlango wa 4, nami ninataka kusoma kifungu cha 17.

Na *tangu wakati huo Yesu alianza kuhubiri*, akisema, *Tubuni: kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia*.

83 Sasa, kwa yapata dakika ishirini ama thelathini za wakati wenu: *Tangu Wakati Huo*. Ninataka kutumia hilo kama somo: *Tangu Wakati Huo*, maneno matatu. Sasa, kuna nyakati, na mambo yanayotukia ambayo hubadilisha mwelekeo mzima wa maisha yetu, tunajua hilo, sote tunajua. Mambo fulani hufanyika katika safari ya maisha ambayo hubadilisha mwelekeo wote wa maisha kwetu.

84 Sasa, kama vile mtoto, huenda ulisema, ulipokuwa mtoto, ya kwamba mambo fulani yalitukia. Nilikuwa na mtu nyumbani . . . Maono haya mnayoyaona hapa jukwaani ni ninii tu . . . hayo kwa kweli . . . ni maono, bali si ono halisi. Hayo ni . . . Hayo ni ninyi mnaofanya hivyo. Si—sio mimi, ni ninyi, unafanya jambo hilo mwenyewe, hulitambui, bali unalifanya. Huwezi kumwelezea Mungu. Mtu yeyote . . . Inakubidi kumwamini Mungu kwa imani. Unapoweza kumwelezea Mungu, si imani tena. Hakuna mtu anayeweza kumwelezea.

85 Lakini ni kama wakati . . . Yesu alikuwa Zawadi ya Mungu kwa dunia. Lakini wakati siku moja Lazaro alipougua, kabla hajawa mgonjwa, Mungu alimwambia Mwanawe, "Ondoka," kisha akamwambia yote yatakayotukia, kwa kuwa Yeye alisema katika Yohana Mtakatifu 5:19, "Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda." Sasa, hiyo haina budi kuwa ni kweli la sivyo Yeye—Yeye alisema uwongo, wala huwezi kumfanya aseme uwongo kwa sababu Yeye ni Mungu. Unaona? Kwa hiyo Baba akamwagiza aondoke. Walituma mtu Kwake wakitafuta msaada kwa ajili ya Lazaro, lakini badala ya kuja, Yeye aliupuuza tu; alijua yatakayotukia, kwa hiyo akaendelea mbele. Wakatuma mtu tena, Naye akapuuza tena. Hatimaye akasema, "Lazaro analala."

Wakasema, "Anafanya vema."

Ndipo akawaambia katika lugha yao, "Lazaro amekufa. Na kwa ajili ye- . . . kwa ajili yenu, nina furaha sikuwapo, lakini ninaenda kumwamsha."

86 Sasa, Yeye alikutana na Martha, naye Martha akasema, "Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa."

87 Na kaburini angalieni, Baba alikuwa tayari amemwonyesha, Akasema, "Baba, ninakushukuru, Wewe tayari umefanya mambo haya. Lakini," Yeye aliomba kwa ajili ya mfano, "Nasema hivyo kwa ajili ya hawa waliosimama hapa. Lazaro, njoo huku." Na mtu, aliyekuwa amekufa siku nne, akafufuka tena kutoka kaburini, tunaamini hilo, Injili. Kamwe hakusema lolote kuhusu kuwa dhaifu, bali maskini mwanamke mmoja aligusa upindo wa vazi Lake, Naye akasema amekuwa dhaifu.

88 Ilikuwa ni kitu gani? Huyo alikuwa ni Baba akitumia karama Yake. Na hilo lilimpandisha juu, na kumwonyesha yale yatakayotukia, na yale yatakayotokea, na kadhalika. Na basi hilo lilikuwa ndilo, Yeye aliendelea na kuliigiza tu kama mchezo wa kuigiza.

89 Lakini mwanamke huyu, yeye, katika imani yake, alikuwa akitumia karama ya Mungu. Akasema, “Kama nikiweza tu kumgusa Yeye.” Mnaona? Na ilikuwa ni yule mwanamke . . . Yesu hakujua ni nani aliyetenda hilo. Akasema, “Imani yako . . . ” sio, “Nimefanya . . . ” bali, “Imani yako imekuokoa.” Mnaona? “Imani yako . . . ” Si imani *Yake*, imani ya *huyo* mwanamke, na hiyo ndiyo sababu ilimdhoofisha.

90 Sasa, katika mikutano na wale wanaotoka na kufuata kila mahali, na wanajua jinsi tu ambavyo Roho Mtakatifu . . . mambo haya hapa, huenda yakakufanya ushuku, lakini—lakini kama ungetoka wakati mmoja na kuangalia yanayotukia, na kuona tu jinsi anavyotabiri hasa . . .

91 Nami ninamwuliza mtu yeyote jambo lolote ambalo alipata kusema, maishani mwangu mwote, ila lililotukia jinsi tu alivyosema lingetukia. Hiyo ni kweli. Ninalielezea miezi na miezi kabla, hasa kabisa. Ni wangapi waliokuwa hapa nilipopitia Washington kwa mara ya kwanza miaka kadhaa iliyopita? Mnakumbuka, ingenibidi kuwashika watu kwa mkono wangu, na kusimama pale na kuwashikilia ili tu nijue ilikuwa ni kitu gani. Nami nikawaambia ninyi nyote basi kwamba Yeye aliniambia kama ningekuwa mwaminifu, kwamba ningejua siri yenyewe ya moyo. Ni wangapi wanajua mimi nikibashiri jambo hilo? Hilo hapo. Mnaona? Je, lilitukia? Hasa kabisa. Mnaona?

92 Nami ninangojea sasa hivi. Kwa nini ninafanya mikutano hii namna hii? Ninasitasita, nikingojea kuona hatua inayofuata ni ipi. Hiyo ni hakika. Sijui nielekee upande gani. Ninaenda kwenye huduma za kimishenari baada ya hapa, nikishangaa tu, maana ninajua tuko mwisho kabisa. Mnaona? Karibu kiasi gani? Sijui, lakini ninaamini tuko mwisho.

93 Mambo fulani yalitukia. Nilipokuwa mvulana mdogo Yeye alinena nami, akasema, “Kamwe usivute sigara wala kunywa pombe, wala kuuchafua mwili wako, kuna kazi utakayofanya nitakapokuwa . . . utakapokuwa mkubwa zaidi.” Liko kwenye kitabu kule nyuma, mnaweza kukisoma. Ndipo mama yangu na hao wengine, walidhania mimi, ni wasiwasi tu.

94 Ndipo ikaendelea, basi siku mbili, siku tatu baadaye, akanielezea jinsi daraja hilo lingevuka mto, chini tu ya mahali petu sasa, watu kumi na sita wangepoteza maisha yao juu yake, nao wakayaandika, ndipo miaka ishirini na miwili tangu hapo likatukia vivyo hivyo hasa, nao watu kumi na sita wakapoteza maisha yao. Haijawahi kuwa, kati ya maelfu ya mambo, bali

limekuwa sahihi kabisa. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mnaona, mambo haya hutokea wakati ukiwa mtoto, hilo linavutia.

95 Sasa, wakati, kadiri wakati unavyosonga mbele, mara kwa mara mambo yanatukia ambayo yanaacha athari kwenye maisha yetu. Kwa mfano, kama tusemavyo, yule mwanamke mzinzi. Nilikuwa nao katika maungamo. Nilikuwa na mmoja si muda mrefu uliopita, kilikuwa ni kisa cha kusikitisha sana. Kwenye nyumba moja, tuliketi pale, nao . . .

96 Watu hupiga simu, huingia kutoka kote ulimwenguni. Mdhamini wa kanisa letu . . . Na baadhi yao wako humu jengoni usiku wa leo. Wanajua ni kweli. Kuna yapata mia tatu kwenye orodha ya wanaongojea, nao wanakuja kutoka Afrika, kutoka Asia, kutoka Ulaya, kutoka kila mahali nilikokuwa, wakingojea, wakiangalia, wanaendelea kuwasiliana nasi mpaka watakapopata wakati. Nasi tunaketi papo hapo mpaka Roho Mtakatifu atakapofunua kila kitu, kisha anawaambia tu la kufanya na jinsi ya kulifanya. Wala hakuna kamwe, wakati mmoja, lilipowahi kushindwa. Mnaona?

97 Mtu huyo anaingia na kungojea, labda ni kitu fulani maishani mwao. Wanajua mpango wa wokovu na kadhalika, lakini kuna kitu ambacho hawajui waelekee wapi au wafanye nini. Nao wanangojea kule miezi kadhaa, wakingojea litukie. Mnaona?

98 Nami nilikuwa na mwa—mwanamke aliyekuja wakati mmoja. Haikuwa nyumbani, ilikuwa mkutanoni. Basi huyo mwanamke . . . Niliingia kwenye wodi ambamo walikuwa na wendawazimu waliofungiwa, na hiyo ilikuwa . . . nikaingia mle. Nao hawangeweza kuwa huko nje hadharani, walikuwa wendawazimu, na—na wengine wao iliwabidi kulindwa.

Ndipo basi, nilipoingia, kijana mwanamke mzuri alikuwa ameketi pale, msichana mrembo, nami nikasema, "U hali gani?"

Akasema, "Njema? Wewe ni Ndugu Branham?"

Nikasema, "Naam." Nami nikasema, "Vema, sijui nianzie wapi."

Akasema, "Laiti ungeanza nami."

Nami nikasema, "Ati wewe?" Nikasema, "Kwani wewe ni mgonjwa?"

Akasema, "Naam, bwana."

Nikasema, "Hii ni ya wendawazimu tu."

Akasema, "Hivyo ndivyo nilivyo mimi." Nikasema . . . Akasema, "Waweza kusikiliza hadithi yangu?"

Nami nikasema, "Bila shaka, mama."

99 Na yale mwanamke huyo aliyoniambia! Kijana, yapata umri wa miaka ishirini na mitano, ishirini na miwili ama ishirini na mitano, kitu kama hicho nadhani, mwanamke mrembo sana,

basi ilionekana kana kwamba angemfanyia mwanamume yeyote malkia mdogo wa kupendeza, mrembo.

100 Naye aliniambia ya kwamba wakati alipolelewa katika nyumba ya Kikristo, basi alipofanya hivyo, alianza kuambatana na mvulana aliyevuta sigara na kunywa pombe, halafu usiku mmoja akapewa kinywaji kilichotiwa kwa siri dawa za kulevya, si hasa pamoja na kitu fulani cha kumwangamiza, bali kitu ambacho hakuninii...vema, yeye...ilikuwa ni kitu fulani... tendo la uasherati. Alifikiri angeyatupilia mbali maisha yake.

101 Akawa mlevi sugu, akawa kahaba. Alichukuliwa, na kupelekwa kwenye Makazi ya Mchungaji Mwema alipokuwa na yapata umri wa miaka kumi na mitano tu, taasisi ya Katoliki, akabadilisha dini yake kutoka kile alichokuwa akawa Mkatoliki. Akarudi, akafikiri angekuwa mzima, akasema jambo lile lile likatukia.

102 Ndipo akachukuliwa, alikuwa anakuwa mtu mzima wakati huo, alichukuliwa na kufungwa miaka miwili katika gereza la wanawake. Na hapo walidhania walikuwa wamemshughulikia vizuri wakati huo. Kasema alipotoka, akasema, jambo lile lile likaanza tena moja kwa moja.

103 Ndipo nikasema, "Vema, sasa, mama, ni...unajaribu tu kufungua ukurasa mpya, hilo—hilo halitafaa kitu." Nami nikasema, "Huenda likasikika la mtindo wa kale lakini," nikasema, "ninataka kukuuliza jambo fulani." Nikasema, "Hivi hutarajii kuolewa, ukiwa mwanamke mrembo kama wewe, na kuwa na mume, na watoto wachanga kama mwanamke yeyote wa kawaida?"

104 Akasema, "Naam, lakini ni nani ulimwenguni angenikubali?" Kisha akasema, "Ningemwahidi nini mwanamume?" Kasema, "Mimi hushikwa na vipindi vya hasira kali," kasema, "ninge—ningepigana, na—na kuapa, na kunywa." Kisha kasema, "Ningeingia ulevini na nisingekuja nyumbani kwa mwezi mmoja." Kasema, "Mwanamume angetaka nini na mwanamke kama mimi?"

105 Nami nikasema, "Asingetaka. Lakini," nikasema, "hivi uliwahi kuwazia kwamba badala ya kuwa kitu tu ambacho shule, ama kugeuza karatasi mpya, ama kitu fulani kinachoweza kukusaidia, kwamba ni ibilisi?"

Naye akasema, "Bw. Branham, daima nimeamini hilo." Akasema, "Sasa, wanasema mimi ni mhuni."

Nikasema, "Siamini hilo. Ninaamini ibilisi amekushika."

Naye akasema, "Daima nimeamini hilo."

Nikasema, "Sasa, njia pekee ya kumwondosha pepo ni katika maombi." Nami nikasema, "Sasa, hebu tupige magoti tuombe."

106 Naye akaomba. Naye akaomba pale kwa muda kidogo, nikaomba pamoja naye, naye akaangalia nyuma, ndipo akasema, "Loo, Bw. Branham, na—naamini ninaondoka hapa, niwe msichana tofauti."

107 Nikasema, "La. Utatoka jinsi ulivyoingia. Unaona? Unalichukulia tu kwa dhana ya kiakili." Nikasema, "Huna budi kuwa makini Dada, na Mungu."

108 Ndipo tukashuka kule chini, na kuanza kuomba, baada ya kitambo kidogo akagonga kitu Fulani. Ndipo akageuka, huku machozi yakitiririkia mashavuni kutoka kwenye hayo macho makubwa ya hudhurungi, akasema, "Ndugu Branham, kamwe sitafanya hivyo tena." Loo, alikuwa amepata Kitu fulani wakati huo.

Ameolewa sasa na ana watoto wawili au watatu. Hajawahi kunywa tangu siku hiyo, hajawahi kuvuta sigara, mnaona, jambo fulani lilitukia.

109 Lakini mnaona, ilianza wakati alipokuwa msichana tu, tendo baya. Mvulana mdogo, labda maskini Elvis mamboleo mwenye mtindo wa kukata nywele kiduku, na—na, huko nje, akifikiri yeye ana sura nzuri sana, ama kitu kama hicho, na muda si muda mwajua, amkumbatie msichana namna hiyo, na kisha afanye hila namna hiyo, huyo ni Yuda wa kisasa. Hiyo ni kweli. Sasa, hakukusudia kufanya hivyo, lakini ilianza kama mtoto.

110 Walevi, nimekutana na wengi wa wale waliosema, "Ndugu Branham . . . " kwenye maskani ya wasokwao na kadhalika.

111 Nilipokuwa New York si muda mrefu uliopita, sitakuwa na wakati wa kulisimulia, bali jinsi ambavyo nilimwokota mlevi. Alikuwa rais wa benki ambayo ningeweza kuiona kutoka mahali alipokuwa, kasema, "Nilikuja nyumbani usiku mmoja, nikakutana na barua ya 'Mpendwa John', nilifikiria ningekunywa pombe niisahau, mimi hapa. Je, unaweza kunipa robo ninunue pombe?" Na haya basi, hawakukusudia kufanya hivyo.

112 Mvuta sigara, mwanamke yule aliyevuta sigara yake ya kwanza, hakumaanisha kuwa mtumwa wa tumbaku. Mvulana huyo, mara ya kwanza ulipovuta sigara hiyo ndogo ya hariri ya mahindi, hukumaanisha, kuwa mtumwa wa sigara. Pombe kidogo ya kwanza uliyokunywa, hukukusudia kuwa mlevi. Unaona, hukusudii kufanya hivyo, bali ilianza kwa sababu mtu fulani alikushawishi kufanya hivyo. Jambo ndilo hilo.

113 Loo, juu ya hadithi za miaka hii thelathini na mmoja kuzunguka ulimwenguni, na kuzunguka, na kuzunguka, nikisikia maungamo, na kadhalika, ingesimamisha nywe—nywele kichwani mwako! Kuwazia juu—juu ya mambo ambayo, kuwasikia wakikiri yale waliyoanza, jinsi walivyokuwa hawana hatia, na jinsi dhambi inavyoonekana nzuri, na jinsi inavyoonekana kuwa ya kuvutia, bali ni—ni njia ya mauti,

usiipitie, chochote ufanyacho. “Jiepusheni na namna yoyote ya uovu.”

114 Mwongo, kamwe hakuninii. . .alidhani angemwambia uongo kidogo mama yake. Alienda akala kahawa kidogo, kisha—kisha akaenda na kupulizia pumzi yake usoni mwa mama yake, “Unaona, ka—kamwe—si—sikuvuta sigara, mama,” bali ulisema uongo.

115 Kimulimuli chekundu kinamulika, “Usifanye *hivi*, mvulana mdogo.” Si rahisi kwenda kuzimu, inakubidi kupiga vita upate kwenda kuzimu. Kila unapokosea, kuna taa ndogo nyekundu inayoingia ndani yako, na kuhesabu kinyumenyume kunakuja, “Ewe mvulana mdogo, usifanye *hivi*.” “Ewe msichana mdogo, usifanye *hivyo*.” Unaona, ni jambo fulani linalofanyika ndani yako, bali unapiga vita moja kwa moja juu yake.

116 Unapita kanisa, na unawasikia watu wakiimba nyimbo za Injili, kweli unataka kuingia, lakini loo, jamani, unawasha sigara nyingine na kutikisa kichwa chako. Unajaribu kufanya nini? Unapigana moja kwa moja kupitia kila kizuizi.

117 Mungu hakupeleki kuzimu, unajipeleka mwenyewe kuzimu. Unavunja kila kizuizi, unapita mbio kwenye kila taa ya kusimamisha ukijaribu kujipeleka mwenyewe kuzimuni. Halafu useme ati Mungu ni mwema wala hatakupeleka kuzimuni? Unajipeleka mwenyewe kuzimuni. Mungu hampeleki mtu kuzimuni, iliumbwa kwa ajili ya ibilisi na malaika zake, si kwa ajili yako. Lakini unapigania kuingia moja kwa moja humo, wanaume na wanawake hufanya hivyo.

118 Mnaona hayo maajabu ya Mungu, (Watu wengine watafanya hivyo.), na kwa sababu tu ya theolojia, kanuni fulani ya imani ya kanisa ama kitu fulani, utaondoka na kumwepuka Mungu usije ukampokea Roho Mtakatifu. Unawaona watu chini madhabahuni wakiomba, unaona hao wanawake wakisimama, na wanaume, na nyuso zao zimeoshwa kwa machozi, na kupiga mayowe, na kutembea huku na huku jengoni, baadhi ya marafiki wako huko nje wakicheka, unasema, “Kama huko ndiko kuzaliwa upya, sitaki uhusiano wowote nako. Kanisa letu linaamini katika kuzaliwa upya, nasi tunaandika tu jina letu kwenye kitabu.” Unaogopa hilo.

119 Hebu niwaambie hili: sijali ni kuzaliwa kwa namna gani, ni mchafuko, kama kuko kwenye zizi la nguruwe, ama katika chumba cha hospitali, kilichopambwa kwa waridi, ni mchafuko. Na kuzaliwa upya si kitu pungufu, bali inahitaji huko kuleta Uzima; huna budi kufa kusudi uzaliwe mara ya pili. Ni kweli.

120 Angalia jinsi ambavyo Mungu anaonya, “Usiseme uongo.” Ndipo kila Mwaka Mpya utatia sahihi nadhiri, “Sitafanya hivyo tena.” Loo, mna nia njema. Bila shaka. Kuzimu imesakafiwa na hizo, na nia njema. Huwazii kwamba. . .Unafikiri hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo, kudhania tu kwamba hivyo ndivyo

unavyopaswa kufanya. Kila Mwaka Mpya useme tu, “Vema, nitafanya nadhiri zangu za Mwaka Mpya, nitaziandika zote,” na kabla ya siku mbili kwisha, tayari umevunja nusu yake. Unaona, huwezi kufanya hivyo.

121 Unatupa ninii yako . . . pakiti ya sigara na kuangalia mahali zimeangukia; unatupa chupa yako mahali fulani na kuhakikisha huivunji, unaiweka kwenye rafu na kumwambia mkeo, “Sitafanya hivyo tena,” unamwambia mumeo, “Sitakunywa pombe tena.”

122 Lakini unaangalia kile unachofanya nayo, maana unairudia moja kwa moja tena, kama nguruwe kwenye kugaagaa kwake na mbwa kwenye matapiko yake. Haina budi kuchukua kitu tofauti; huna budi kufia kiumbe ulicho. Unaona? Naam, bwana.

123 Huanza kama mtoto asiye na hatia, labda katika nyumba nzuri ya Kikristo, lakini kulikuwa na mtu aliyekuja, maskini mdowezi alikuja na kukupotosha kutoka kwenye barabara nzuri. Unaweza kujua hasa wakati lilipoanza, wakati ulipoanza kusema uongo kwa mara ya kwanza, wakati ulipoanza kuiba, ulipoanza kunywa pombe kwa mara ya kwanza, wakati ulipoanza kufanya jambo lolote baya.

124 Kabla hujaweza kukubali makosa, huna budi kukana yaliyo mema. Huna budi kukana moja kwa moja mbele zako . . . Huna budi kukana Kweli ya Mungu kabla hujaweza kukubali chochote kibaya. Hiyo ni kweli kabisa. Angalieni. Sasa, katika Mwaka Mpya, unabadilika na kusema, “Sasa, ni . . . nitafungua ukurasa mpya.” Una nia njema. Bila shaka. Ninaamini taifa lina nia njema.

125 Naweza tu kukumbuka kwa shida, kama mvulana mdogo, yapata umri wa miaka mitano, wakati Vita vya Kwanza vya Dunia vilipoanza. Najua baba yangu alipanda barabarani akiwaendesha farasi wawili katika mkokoteni wa springi, naye alikuwa na gunia la maharagwe na unga kidogo (alikuwa kwenye duka la vyakula), ameketi ki—kitini. Nami nikamsikia, akashuka kwenye mkokoteni, akaingia ndani.

Ndipo mama akasema (huko chini kabisa mjini, maili kadhaa huko chini), kasema, “Nilisikia filimbi zikilia kabisa.”

126 Akasema, jina lake lilikuwa Ella, kasema, “Ella, wametangaza vita.” Naye alikuwa na umri wa takriban miaka ishirini na miwili, kasema, “Mnajua hilo linamaanisha nini? Ninaenda.”

Ndipo nikaokota gunia hilo la maharagwe, nikasema, “Wakimfuatilia baba yangu, nitawatwanga kwa gunia hili la maharagwe.” Nilikuwa—nilikuwa mdogo sana, lakini mimi . . .

127 Akasema, “Sasa, wanatwambia, kama tutaenda ng’ambo na kuvipiga vita hivi, hakutakuwa na vita tena.” Kisha kasema, “Huyu hapa Billy, huenda ikamlazimu kwenda siku moja; kuna

Edward, huenda ikamlazimu kwenda; kuna Melvin, huenda ikamlazimu kwenda." Nami nikasema, "Kama nikienda na kuwasaidia kupigana na kuwapata, wawe huru tena," kasema, "wanatwambia hakutakuwa na vita tena, na itamaliza vita watakapokuwa na Vita hivi vikuu vya Dunia."

Walikuwa na nia nzuri walipokuwa wakisema hivyo, lakini walitokea moja kwa moja tena na nyingine. Naam, bwana.

128 Waliunda, kile walichokiita Shirikisho La Mataifa baada ya kitambo kidogo, polisi. Wakasema, "Tunalo wazo sasa," nia njema, "tuna Shirikisho La Mataifa, na tutakapofanya hivyo, tutaulinda ulimwengu mzima kwa hilo." Huwezi kufanya hivyo, lilishindwa kabisa.

129 Wana U.N. sasa. Hawastahili mkataba ulioandikwa juu yake. Hiyo ni kweli. Bila shaka. Wakati hawatakubali maombi, na kuchukua njia nyingine yoyote ya kutokea ila njia ya Mungu, vema, li—linaweza kudumu kwa muda gani?

130 Wana nia njema, lakini haidumu kamwe. Bila shaka haidumu. Litaanguka chini kabisa, na kuingia katika historia mavumbini. Vema, mnaona mahali lilipo sasa hivi. Ulimwengu mzima unatetemeka, basi U.N. inafaa nini? Ni jina tu. Hiyo ni kweli.

131 Hakuna taifa lililowahi kufanywa kulitawala lingine, Mungu alimwumba mwanadamu, naye mwanadamu akawafanya watumwa. Hatupaswi kuwa watumwa, tunapaswa kuwa ndugu. Hivyo ndivyo Injili inavyotufundisha, kuwa ndugu.

132 Hili hapa kanisa linakuja likiwa na nia njema, waliwazia, "Tutafanya ninii . . . dhehebu hili kuu. Tutawaelimisha wahubiri wetu, tutawaadibisha sana na kila kitu, nao watawafundisha watu, wala hakutakuwa tena na watu wasio na elimu katika nchi yetu."

133 Nasi tulifanya nini? Tuna kundi la makafiri wenye elimu, wasioamini tena, kwenye Neno la Mungu. Kila kitu ambacho . . . Mwanadamu daima amejaribu kufanikisha jambo fulani peke yake, bali kamwe hajaweza kulifanya. Nimrodi alijaribu kutengeneza mnara ambao angeweza kuupanda kwenda Mbinguni, ukaanguka mavumbini. Nebukadreza alijenga mji, usiopatikana na mauti, wa Milele, alivyowazia, ukaingia mavumbini.

134 Wamarekani, wakimwonea wivu dada yao, Uingereza, walijenga meli iliyoitwa Titaniki ambayo "haingeweza kuzama." Mungu kwa mkono Wake wenye nguvu aliuonyesha ulimwengu haiwezi kusimama.

135 Ninii . . . Ufaransa walidhani wangeweza kuishi katika dhambi na kufanya Ngome ya Siegfried. Ilifaa nini? Wajerumani walizunguka moja kwa moja nyuma yake na kuiteka.

136 Wajerumani walijenga Ngome ya Maginot na kusema, “Tuna kitu ambacho hakuna mtu, anayeweza kuingia ndani yake.” Nao Wamarekani wakailipua kwa mabomu ya makombora. Hiyo ni kweli. Inaonyesha ya kwamba mafanikio ya mwanadamu ni bure, kwa sababu mawazo yake yamepotoka, wala hawezi kusimama. Yote ni nini? Kuna kitu mle ndani kinachoonyesha kuna Mji wa Milele hata hivyo. Hiyo ni kweli.

137 Mume na mke vijana, walipofunga ndoa, nimekuwa nao kwenye maungamo, mara nyingi nawashika kwenye mstari wa maombi, nao wanasema, “Vema, Ndugu Branham, mimi na Yohana tulifunga ndoa, tulikuwa tunataka kujenga makazi, na ilikuwa ni sawa, mpaka siku moja mkusanya bima, ama—ama mwuza vitabu, alipokuja mlangoni, na—naye akauliza kama ningeweza kuingia ndani tu. . . kama angeweza kuingia kwa dakika chache, nikamruhusu tu. Na tangu wakati huo,” mnaona, “hapo ikaanza.

Mwanamume anaweza kusema, “Ndugu Branham, nilikuwa na mke mzuri, ni—nilikuwa na familia nzuri, ndipo siku moja tukamwajiri msichana mpya wa ofisini . . . ”

“Nilikuwa huko chini bustanini, nikakutana na maskini mama mmoja, alikuwa amevaa kaptura, akanijia. Tangu wakati huo.” Mnaona?

138 Kuna wakati ambapo wewe unaanza. Naam. Kulikuwa na wakati ambapo mambo haya yote yalianza. Kulikuwa na wakati ambapo mauti yalianza, hapo ndipo Hawa, akitembea siku moja katika bustani ya Edeni, alikutana na Shetani. Naye Shetani . . . Wakati Mungu alipokuwa na Kanisa La—Lake . . .

139 Watu wanapoenda vitani wanachunguza vitu vya ku—kushambuliana. Wakati walipomvika kurutu chepeo kwa mara ya kwanza, alidhani hicho ndicho kitu kibaya sana alichopata kuwa nacho, na kubeba mkoba wa ratili tisini mgongoni mwake, bali alipofika huko nje vitani, alihitaji kila chombo.

140 Alipomvika chepeo, hiyo ilimaanisha kwamba ilimbidi, alihitaji hiyo chepeo, kwa sababu kutakuweko na marisau. Kamwe hakuwa nayo hapo awali, bali ilimbidi awe nayo wakati huo, kwa sababu ilihitajika, walikuwa wameisomea.

141 Kila mwaka wanajifunza kitu tofauti, wanapata kitu kikubwa zaidi, kwa sababu cha kale hupitwa na wakati. Ndege zetu nzuri tulizokuwa nazo katika vita vya mwisho vya dunia ni vikorokoro, vyenye thamani ya mabilioni ya dola. Injini ya kale ya mvuke imepitwa na wakati. Bila shaka. Bunduki tulizotumia, kwanza ile ya kale ya Krag-Jørgensen, na halafu ile—ile ya Springfield, halafu kufikia Garand ya kisasa, na sasa ni kombora la atomiki. Zote zimepitwa na wakati. Tunajaribu kutafuta, tunaendelea kutafuta kitu bora zaidi.

142 Lakini wakati Mungu alipoanza kumwimarisha mtu wake, Yeye alimpa Kitu kilicho bora kuliko vyote, wala haimbidi

kukibadilisha tena, Yeye alimpa Neno Lake. Amina. Hiyo ndiyo Ngome yake: Neno la Milele la Mungu.

143 Ndipo adui alijongea karibu, wapelelezi . . . Tuna wapelelezi wa Kiingereza hapa, na—nasi tuna wapelelezi huko Uingereza. Kote ulimwenguni tuna wapelelezi, nao wana wapelelezi kutoka kote ulimwenguni humu ndani. Wanajaribu kufanya nini? Kutafuta yale tumejaribu kufanikisha.

144 Naye ibilisi hufanya kazi vivyo hivyo. Anakuja kujaribu kupata kitu fulani, kile Mungu amefanya, kisha anajaribu kutafuta kitu cha kukabiliana nacho. Lakini Mungu kamwe hana haja ya kubadilisha Chake, kwa sababu Yeye aliwapa Neno Lake hapo mwanzo. Yeye hana kikomo, hawezi kubadilika. Nalo lingali ni Neno Lake siku hizi, kamwe halibadiliki kutoka kwenye Neno Lake. Huyo hapo katika Neno Lake. Kanisa Lake limeimarishwa kwa Neno. Mtu Wake wa kwanza alikuwa ameimarishwa, Hawa. Lakini aliposimama kwa dakika moja tu kusikiliza mbinu za Shetani . . .

145 Mbinu za Shetani ni nini? Kutoa hoja, "Ni jambo la busara tu . . . " Basi unaposikia jambo lolote linalotoa hoja dhidi ya Neno, liondokee, ni ibilisi. Sijali ni la mtindo wa kale jinsi gani, jinsi linavyoonekana la kigeni, wakati Mungu aliposema hivyo, hilo latosha Milele. Ondokea chochote kinachotoa hoja dhidi ya Neno.

146 "Loo, ni jambo la busara, leo hii, hatuhitaji uponyaji wa Kiungu, kwa sababu tuna madaktari wazuri." Liondokee hilo. "Ni . . . Loo, ni wale mitume kumi na wawili tu waliompokea Roho Mtakatifu. Ni . . . "

Vema, kwa nini Petro alisema? "Ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie."

Jamaa fulani alisema, "Ilikuwa ni kwa ajili ya *kule* nyuma tu."

147 Nikasema, "Umechelewa kupita kiasi, tayari nimeipata *hapa* chini," kwa hiyo—kwa hiyo sisi—kwa hiyo tunajua ni sahihi. Mnaona? Chochote kinachotoa hoja dhidi ya Neno la Mungu . . . Kasema, "'Ishara hizi zitafuatana na hao, waaminio.'" Jinsi gani? "'Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye . . . '" ulimwenguni kote wakati wote. '"Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.'"

148 Umbali gani? Ninaweza kuwaonyesha mahali ambapo Mungu aliweka uponyaji wa Kiungu Kanisani. Sasa, ninyi nionyesheni mahali alipouondoa kwa Neno. Mnaona? Miujiza na ishara, na Roho Mtakatifu, ni Yesu yeye yule jana, leo, na hata milele. Bila shaka.

149 Sasa, tunaona, kama—kama Shetani angeweza kumfanya Hawa kutoa tu hoja kwamba Neno hilo lilikuwa . . . Kasema,

"Sasa, hakika hamtakufa. Loo, hakika, Mungu amesema, hiyo ni kweli kabisa, lakini hakika . . ."

150 Hicho ndicho kitu cha kwanza alichoshinda kwacho, na hicho ndicho kitu ambacho angali . . . aliiangusha jamii ya binadamu kwake, kutoa hoja. Yeye huiua jamii ya binadamu kwa kutoa hoja dhidi ya Neno Lake.

151 Nazo seminari kuu na kadhalika zinainuka, nao wanaweka nia zao pamoja na kutoa hoja, na mambo kama hayo. Sijali kuna wangapi wenye akili, "Neno la kila mtu na liwe uongo na la Mungu liwe Kweli." Sawa.

152 Angalieni, Mungu hushughulika na mtu binafsi. Basi angalieni, lakini kila wakati kukiwa na jambo fulani: "Tangu wakati huo."

153 Tangu wakati ambapo Hawa alisikiliza hoja za Shetani, mauti iliingia ulimwenguni na imetawala tangu wakati huo. Kumbukeni, msisahau mahali hapo ambapo Hawa . . .

154 Kulikuwa na wakati ambapo hapakuwapo na mauti duniani, kulikuwa na wakati ambapo haikuwalazimu wanadamu kufa. Lakini kwa sababu kwamba Hawa alihoji, akasikiliza hoja za Shetani dhidi ya Neno la Mungu, mauti ilianza kutawala tangu wakati huo na kuendelea, nayo ingali inatawala hata leo.

155 Lakini hebu niseme hivi: Mbele ya hayo yote, kuna wakati, na jambo linaloweza kutukia ambalo halitabadilika kamwe, ni la Milele. Kuna jambo linaloweza kutokea katika maisha ya mwanadamu ambalo haliwezi kubadilika kamwe, hilo ni la Milele, hapo ni wakati mtu anapokutana na Mungu. Hilo limetatuliwa Milele, mtu anapokutana na Mungu, amezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, yuna Uzima wa Milele. Sasa, tunaamini hilo kwa moyo wetu wote.

156 Basi kumbukeni, wakati mwanamume huyo, mwanadamu, ama mwanamke huyo, mvulana huyo, ama msichana huyo, akiwahi kukutana na Mungu na kubadilishwa, yeye si yule yule kamwe, anabadilishwa tangu wakati huo na kuendelea. Hiyo ni kweli. Kamwe hatakuwa vile vile, haidhuru, huenda akamwacha Mungu, bali Mungu kamwe hatamwacha. Kila uendako, utasumbuliwa mchana na usiku kama ukiwahi kukutana na Mungu, mpaka utakaporudi tena. Hiyo ni kweli.

157 Aliyerudi nyuma ndiye maisha yenye mashaka kuliko yote yaliyopo, na kwa hiyo, yatakusumbua mchana na usiku. Ni mara ngapi tumesikia maungamo yao na kadhalika, jinsi walivyo na mashaka, na masikitiko, yote hayo! Kama walifanya hivyo, wanajua inawabidi kuvuna hasa kile walichopanda. Pia kumbukeni, unapanda punje moja na kupata suke zima lililojaa hayo. Unaona? Kwa hiyo tunajua ya kwamba kutakuwa na mavuno mengi kwa upanzi ule uliofanya. Na . . . Lakini mtu anayekutana na Mungu kamwe si yule yule. Hebu tuchukue watu wachache sasa, kabla hatujafikia mahali tunapotaka.

158 Hebu na tuchukue, kwa mfano, Ibrahimu. Alikuwa tu ni mtu wa kawaida. Alishuka kutoka... Babeli pamoja na baba yake, naye akaishi... aliishi katika nchi ya Wakaldayo, katika mji wa Uru, labda mkulima, mtu wa kawaida. Hakuwa mtu maalum, alikuwa ni mwanadamu tu, naye akapata neema machoni pa Mungu.

159 Naye Mungu akamwambia, alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, ya kwamba angemfanya kuwa baba wa mataifa, na kwamba atampa mtoto kwa mke wake Sara, ambaye alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano wakati huo. Ndipo Ibrahimu akamwamini Mungu, naye akahesabiwa kwamba ana haki.

160 Ibrahimu alibadilishwa. Basi angalieni, mtu anapokutana na Mungu... Mungu alimwita Ibrahimu, Naye akamwambia alitaka ajitenge na jamaa zake wote wasioamini. Ndipo Mungu anapomwita mtu kumfanyia kazi, Yeye anakuita kutoka kwenye maangamizi kamili kutoka kwa mambo yote ya ulimwengu, na dhambi za dunia; utengano.

161 Mungu kamwe hakumbariki Ibrahimu mpaka alipomtii kikamilifu. Alimchukua baba yake, huyo mzee sikuzote alikuwa ki—kikwazo, ama, samahani usemi huo, lakini sikuzote alikosea, naye... naye Ibrahimu... na halafu akamchukua Lutu, ndipo basi hatimaye akashuka akaenda kule. Na baada ya Lutu kujitenga, ndipo Mungu akamwambia Ibrahimu, "Amka utembee nchini, nimekupa yote, yote ni yako." Mnaona, Yeye kamwe hakumbariki kikamilifu mpaka Ibrahimu alipotii kikamilifu.

162 Wala kamwe hutaweza kupata chochote kutoka kwa Mungu, na kupata kibali cha Mungu, ndugu na dada zangu, popote mlipo, mpaka tutakapolitii Neno la Mungu kikamilifu. Unajifanya mwenye mashaka kwa kulikaribia tu shingo upande. Naam.

163 Lakini Ibrahimu alipokutana na Mungu, alikuwa mtu aliyebadilishwa, alikuwa tangu siku hiyo na kuendelea. Kidogo alitenda kigeni, akakimbia huku na huku... Ninaweza kumwazia Sara, amepata umri wa karibu miaka sitini na mitano, akashona vijiatu, na—na kuchukua baadhi ya jicho-ndege, na lundo la pini, na kusema, "Vema, tutampata mtoto huyo."

Ndipo basi majira ya kawaida yalipokuja ninaweza kumsikia Ibrahimu akisema, "Mpenzi, unajisikiaje? Ni karibu wakati huo."

"Hakuna tofauti."

"Utukufu kwa Mungu, nitampata mtoto huyo kwa vyovyote vile."

Miezi miwili ikapita, "Mpenzi, tofauti yoyote?"

"La, hakuna tofauti."

"Utukufu kwa Mungu, ni mwujiza mkuu kuliko ilivyokuwa mwezi uliopita. Tutampata huyo mtoto kwa vyovyote vile."

Miaka mitano ikapita. "Wajisikiaje sasa, mpenzi?"

"Hakuna tofauti."

"Haleluya! Tutampata huyo mtoto, ni mwujiza zaidi kwa miaka mitano. Utukufu kwa Mungu."

Miaka ishirini na mitano ikapita. "Unajisikiaje, Sara?"

"Hakuna tofauti."

"Utukufu kwa Mungu, tutampata kwa vyovyote vile."

"Unajuaje?"

"Mungu alisema hivyo."

164 Alikutana na Mungu naye akawa mtu aliyebadilika, "Hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; bali alikuwa na nguvu, akimtukuza Mungu."

165 Sasa, tunapaswa kuwa Uzao wa Ibrahimu kama tuna imani ya namna hiyo: Kile Mungu asemacho ni kweli. Mtu anapokutana na Mungu, daima Neno Lake ni kweli. Kama mtu anasema ya kwamba anamwamini Mungu, huku analikana Neno hili, kuna kasoro, maana Roho Mtakatifu ni Mungu, naye Roho Mtakatifu aliiandika Biblia, basi Roho Mtakatifu angewezaje kuwa *hapa* ndani, na kuiandika Biblia, kisha ageuke, aikane? Kuna kasoro mahali fulani.

166 Nawaambia, tukio halisi la Roho Mtakatifu litaitikia kila sentensi ya Biblia hiyo kwa "Amina." Sawa. Haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini, bila shaka atafanya hivyo, kwa sababu ni Roho wa Mungu, Mwandishi wa Biblia. Naye Roho—Roho wa hilo Neno ni Roho Mtakatifu, huyo ndiye anayelihuisha, "Andiko huua, Roho hulipa Uhai," mnaona, analipa andiko, ninii . . . waraka tu ulioandikwa, Uzima, analidhihirisha, anatimiza yale hasa Mungu aliyoahidi.

167 Ibrahimu alikuwa mtu aliyebadilika, mwenye nguvu, wakati wote akimsifu Mungu. Haidhuru alifanya kiasi gani, hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini. Kwa nini? Alikutana na Mungu, alikuwa mtu aliyebadilishwa.

168 Wakati mmoja nabii mtoro, katika dhana yake ya kiakili ya kile Mungu alichokuwa, akijua ya kwamba alikuwa ni mtu aliyeitwa, alikuwa na yote . . . hata angeweza kufundisha hekima ya—ya Misri, naye angeweza kuwafundisha walimu wao hekima, lakini akatoroka, akamwoa maskini msichana mrembo wa Kushi, wakiishi huko nje nyuma ya jangwa, wametulia kabisa, mzigo wa hao watu ulikuwa umekwisha.

169 Hiyo ndiyo shida ya makanisa ulimwenguni siku hizi. Tumepoteza mzigo. Hakuna mikutano ya maombi tena. Hakuna tena . . . Inaonekana kana kwamba imekufa. Sikemei, ninatoa tu tamshi la kweli, ndugu, nanyi nyote mnajua hilo, mnaliona

katika makanisa yenu. Sisi...Ni, jambo fulani limetukia. Hakuna shauku tena, kuna kasoro, Moto umezimika. Katika hekalu la kale la Kirumi la Vesta wakati mioto ilipozima, watu walienda nyumbani, shughuli zilikwisha. Loo, iwasheni Mioto tena, Moto kwenye madhabahu ya moyo wetu! Naam. Loo, tumrudishe Mungu miongoni mwetu. "Mrudisheni Mungu," ndicho kilio chetu.

170 Sasa, Musa tayari amepoteza mzigo wa watu wake. Alikuwa ameshindwa pamoja na dhana yake ya kiakili ya Neno. Naye alikuwa akitembea upande wa nyuma ya jangwa siku moja, na kulikuwa na Moto kichakani. Nuru hiyo iliyokuwa imemfuata ilikuwa katika...ile iliyokuwa imfuate, ilikuwa kichakani. Akaenda kando ya kichaka hicho, akavua viatu vyake, ndipo Sauti ikasema, "Nimeyaona mateso ya watu Wangu." Kuna Mtu ambaye angali anajali, huyo ni Mungu.

171 Akasema, "Nimeyaona mateso ya watu Wangu, nimesikia kuugua kwao, sababu za wanyapara, nami nimeshuka. Ninakumbuka ahadi Yangu." Haleluya! Hawezi kutoa ahadi pasipo kuikumbuka. Amina. Yeye daima, Mungu Milele hukumbuka ahadi Yake. Mungu hutoa ahadi, Mungu daima huikumbuka ahadi Yake. Alisema, "Ninakumbuka ahadi Yangu kwa watu Wangu, nami nimeshuka kuja kuwakomboa, nami ninakutuma wewe." Amina.

Musa akasema, "Mimi ni nani?"

Akasema, "Unaenda."

Akasema, "Lakini siwezi kuzungumza."

Akasema, "Ni nani anayemfanya mtu kuwa bubu au kunena?" Amina. Usihojiane na Mungu. Lichukue tu Neno Lake.

Hebu niwaambie, siku moja kule, Yeye alisema, "Hakika nitakuwa pamoja nawe."

Akasema, "Unionyeshe utukufu Wako."

Akamwonyesha uponyaji wa Kiungu, akamwonyesha jinsi ya kufanya mwujiza. Alikuwa tayari kwenda. Naam, bwana.

172 Sasa, angalieni ni tofauti jinsi gani: Siku moja bingwa wa kielimu aliyeshindwa upande wa nyuma ya jangwa akiwa na—akiwa na kazi ya nyumbani ya kuwalisha kondoo wa baba mkwe wake. Ndipo kesho yake sisi...Nakwambia, unapokutana na Mungu, inakufanyia jambo fulani, inakufanya utende kiwazimu kwa ulimwengu. Mwangalieni kesho yake, anamchukua mkewe, Sipora, anamketisha kutagaa juu ya nyumbu, na mtoto kwenye nyonga yake, huku ndevu zake zimening'inia chini *hivi*, na kichwa chake chenye upara kiking'ara, fimbo iliyopinda mkononi mwake, masharubu yakipepea, akipaza sauti, "Utukufu kwa Mungu! Utukufu kwa Mungu!" Mzee, umri wa miaka themanini.

"Kwani unaenda wapi?"

"Nashuka kwenda Misri kuiteka."

"Ati nini?"

"Nashuka kwenda Misri kuiteka." Uvamizi wa mtu mmoja. Kwa nini? Alikuwa amekutana na Mungu. Na jambo la ajabu ni kwamba, alifanya hivyo, aliiteka.

173 Mungu anataka tu mtu mmoja ambaye Yeye anaweza kumtawala kikamilifu, hiyo ni kweli, mtu mmoja ambaye atajisalimisha kikamilifu Kwake.

174 "Ninashuka kwenda kuiteka." Ni jambo la kipuuzi jinsi gani! Jeshi kama hilo, katika siku hizo, lililokuwa limeushinda ulimwengu mzima, jeshi kubwa kuliko vile lingekuwa leo hii, kama kwenda kukutana na Urusi. Alikuwa na fimbo ya kale iliyopinda mkononi mwake.

"Utalifanya na nini?"

"Fimbo hii pamoja na nguvu za Mungu. Mimi huyu hapa naenda," masharubu yakipulizwa na…huku na huku, na ni mzee, mwenye umri wa miaka themanini.

175 Kwa nini hakufanya hivyo alipokuwa shujaa kijana? Mnaona, ilimbidi Mungu kuiondolea mbali elimu hiyo yote. Ilimbidi kumpeleka upande wa nyuma ya jangwa, na kumpondaponda, na kumvunja, kisha kumrudisha, na kumtokea, na kumwonyesha kile alichokuwa, Naye ali-… Alipokutana na Mungu alikuwa ni mtu aliyebadilishwa. Kwa namna fulani huwafanya watu siku hizi kidogo watende kigeni pia, wakati wanapokutana na Mungu kweli, lakini wanajua mahali wanaposimama.

176 Inanikumbusha wakati nilipokuwa nikiwapiga ndama chapa. Mama yangu alikuwa akisema, nilipokuwa nikipanda farasi kuwakusanya, tungewapiga ndama chapa, angesema, "Loo, Bill, unawezaje…?"

177 Ningepasha moto vyuma mara nyingi, nibebe vyuma hivyo, nisingeweza kupata ujasiri, kuviwekelea juu ya ndama, lakini yeye…Kasema, "Kwa nini unafanya hivyo…?" Kasema—kasema, "Hilo linachukiza sana." Kasema, "Mnafanya nini?"

178 Nikasema, "Vema, tunamfunga tu vilivyo, tunamfinyilia kule chini, na kumchoma kwa chuma cha kutia alama." Nami nikasema, "kumchoma tu moja kwa moja ndani ya ngozi yake, kisha kumpaka lami kidogo, halafu tukamwachilia." Nikasema, "Nusura ashikwe na kifafa, anarusha tu miguu, na kupiga mayowe, na kukoroma, na kuendelea." Lakini, ndugu, yeye anajua yeye ni wa nani tangu wakati huo na kuendelea. Hiyo ni kweli kabisa.

179 Hivyo ndivyo ilivyo kwa Roho Mtakatifu. Kama Mungu akiweza kukufanya utulie vya kutosha kukutia chapa, haleluya, kukutia muhuri katika Mwili wa Kristo kwa Roho Mtakatifu, unajua mahali pako.

180 Tunaishi katika siku kuu ya kuchanganya mbegu. Nilikuwa nikisoma makala katika *Reader's Digest* si muda mrefu uliopita, uchotara huu. Nilikuwa nikishuka, niliona lilisema, "Mahindi chotara, mahindi makubwa mno, masuke mazuri." Hayafai kitu, hayana faida yoyote, ni uharibifu kwako. Nyama chotara, chotara, kila kitu ni chotara, chotara, chotara. Haifai kitu. Hebu chukua mahindi yako chotara, jaribu kuyapanda tena, uone utakachopata. Hayafai kitu.

181 Hata wana dini chotara siku hizi, pia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Walilichukua kwenye maungamo ya kimadhehebu badala ya tukio la Roho Mtakatifu, kuchanganya mbegu.

182 Chotara hufanya nini? Hufanya suke linaloonekana bora, bali halina uhai ndani yake. Hivyo ndivyo, kama likifanya kanisa linaloonekana bora zaidi, bali hakuna Uzima ndani yake, chotara. Hiyo ni kweli.

183 Sayansi inakanusha yao wenyewe, ama, inathibitisha theolojia yao wenyewe, kwamba mwanadamu alitoka kwenye seli moja, kwa kufanya hivyo. Hawezi kujibadilisha na kuwa bora zaidi na zaidi, kwa sababu mara tu alipoichanganya mbegu yake, amekwisha papo hapo.

184 Hebu mchukue nyumbu. Nyumbu ndiye kitu kijinga sana kilichopo. Sikuzote nilimhurumia. Huyo hapo amesimama. Basi angalia, yeye hajui baba, mama yake walikuwa ni akina nani. Mama yake alikuwa farasi, na baba yake alikuwa punda dume. Kwa hiyo hajui yeye alikuwa ni nani. Hajui kama yeye ni farasi ama punda, hajui; yeye ni chotara, kamwe hawezi kujizaa tena, amekwisha.

185 Karibu kama baadhi ya dini hii ya nyumbu tuliyo nayo siku hizi. Nyumbu ni ki—kitu duni sana, ataketi nawe useme *jambo lingine*, kwake namna hiyo, ndipo anatoa masikio yake nje na "Hoo, hoo, hoo!" Mnaona? Hata hajui kile. . .Hakuna upole kwake, yeye ni nyumbu tu.

186 Nawe unaweza kuketi na kuzungumza juu ya ishara kuu za Mungu na Roho Mtakatifu, maskini nyumbu hao wanaketi hapo na kusema, "Hoo! Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama Roho Mtakatifu." Ninyi wasomi chotara! Siwi katili, bali ninawaambieni tu jinsi ilivyo. Loo, yeye hajui baba au mama alikuwa ni nani.

187 Lakini, loo, napenda farasi halisi ukoo safi. Loo, yeye ni mpole, unaweza kumfundisha adabu. Kwamba. . .Ninapenda Mkristo halisi ukoo safi, aliyezaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, sio yule aliyekuwa Mmethodisti jana, Mbatisti kesho yake, na Mpresbiteri kesho yake, na kitu kingine leo *hii*, kila wakati jambo fulani linapoenda kombo kanisani. Lakini mtu halisi aliyezaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, anajua babu zake walikuwa ni akina nani, anajua Baba na Mama yake walikuwa ni nani, anajua alikotoka; amezaliwa na Roho wa

Mungu. Haleluya! Unaweza kumulika Neno la Mungu juu yake na upesi analiona, naam bwana, "Amina," anasema. Sasa, yeye ni kitu kizuri jinsi gani, mfano. Lakini huku kuchanganya mbegu kwote! Naam.

188 Musa, akiwa ni Mkristo ukoo safi sasa, mwaminio, anashuka kwenda Misri, anatenda mambo ya kigeni, ya kipekee sana, bali anajua kilichotukia, kwa sababu kulikuwa na wakati ambapo alikutana na Mungu. Naam, bwana.

189 Kulikuwa na wakati pia ambapo. . .Ninawazia juu ya—juu ya mtu mwingine aliyekutana na Mungu, alikuwa maskini mwanamwali. Alikuwa na kitu cha kuamini, Mariamu. Hakujawahi kuwa na mtoto aliyezaliwa ulimwenguni bila baba na mama, tunajua hilo. Kwa hiyo tunaona ya kwamba Mariamu, maskini mwanamwali, akienda zake kisimani siku moja, Nuru kuu iliangaza mbele zake, akaangalia, amesimama pale kwenye hiyo Nuru, na hapo alisimama Gabrieli, yule Malaika Mkuu, kasema, "Salamu, Mariamu. Umebarikiwa katika wanawake," na kumwambia yale hasa yatakayotukia.

190 Siku chache kabla ya hapo, alikuwa amekutana na kuhani, na. . .mume wa binamu yake, Zakaria, naye alikuwa amesimama madhabahuni akifukiza uvumba, ndipo Gabrieli akatokea na kumwambia ya kwamba alikuwa anaenda nyumbani kuwa pamoja na mkewe na kupata mtoto, na atamwita jina lake "Yohana."

Kasisi huyo alisema, "Hili linawezekanaje? Mimi ni mzee sana, haliwezi kutukia. La, haliwezi kutukia."

Akasema, "Mimi ni Gabrieli, ambaye ametumwa kutoka Uweponi mwa Mungu. Neno Langu litatimizwa katika siku zao. Utakuwa bubu mpaka huyo mtoto mchanga atakapozaliwa."

191 Lakini huyu hapa anakuja kwa maskini mwanamwali huyu. Sasa, Zakaria angekuwa—angekuwa na mi—mifano mingi, kwa kuwa alikuwa amepata ya kwamba kulikuwako na Hana, alijifungua mtoto alipokuwa mkongwe; Sara alijifungua mtoto alipokuwa mkongwe. Mifano mingi katika Biblia, lakini hata hivyo alikuwa asiyejali hilo. Lakini ilimbidi Mariamu kuamini jambo ambalo kamwe halijatukia, bali alikuwa amekutana na Mungu, kasema, "Itakuwaje?"

Kasema, "Roho Mtakatifu atakutia uvuli. Na Kitu hicho kitakachozaliwa ndani yako, kitaitwa Mwana wa Mungu."

Akasema, "Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana." Ati nini? Alikuwa amekutana na Mungu.

192 Asingeweza kutulia, nafikiri aliirudisha hiyo jagi nyumbani, kisha akaondoka kwenda kushuhudia kila mahali, huku maskini mashavu yake yakiangaza, akisema, "Nitapata mtoto. Nitapata mtoto," akipanda vilima vya Yuda.

193 Alisikia kuhusu binamu yake, Elisabeti, alikuwa anaenda kupata mtoto huko juu. Na kwa hiyo, ninaweza kuwazia... Mwajua, alikuwa amejifungia sasa kwa muda mrefu sana. Alikuwa na yapata miezi sita, kwa Elisabeti. Kuna tofauti ya miezi sita kati ya Yohana na Yesu.

194 Na kwa hiyo, alikuwa amefungiwa kwa yapata miezi sita, akakaa ndani, si kama baadhi ya wanawake hawa siku hizi, samahani, mngemsikiliza daktari wenu, nami ni ndugu yenu. Lakini, waangalieni wanawake hawa wajawazito hapa nje wamevaa maskini kaptura hizi, na ki-...ni aibu kwa binadamu. Kusema kweli, siamini mbwa angefanya hivyo. Na hapo, wanawake hawa hapa nje wakitenda hivyo, ndi—ndicho kitu cha kuhuzunisha sana nilichopata kuona maishani mwangu, kitu cha aibu sana.

195 Halafu basi mvulana fulani anawaona wasichana wenu huko nje namna hiyo, halafu hebu awatusi, na basi mnataka kumpeleka gerezani. Wewe ndiwe uliyesababisha hilo kwa kumtuma nje namna hiyo.

196 Nanyi wanaume unamwacha mkeo atoke nje namna hiyo, aibu kwako! Kuna shida gani? Hivi huna heshima zaidi kwa mke wako kuliko hiyo? Sasa, la, sitaki kuingilia hilo. Angalieni. Hilo ni jambo baya kwangu. La. Ninawapoteza marafiki wengi kupita kiasi, bali ninajua ninadumu katika urafiki na Kristo, kwa sababu imeandikwa papa *hapa*. Hiyo ni kweli kabisa.

197 Na hapa, Elisabeti alikuwa amejificha. Ndipo wakati maskini Mariamu...Ninaweza kumwona akija njiani, kwa nguvu awezavyo, mwajua. Naye Elisabeti alikuwa huko nyuma akitengeneza vijibuti vidogo na kulia, kwa sababu maskini Yohana, mwajua, alikuwa—alikuwa na miezi sita, naye alikuwa amekufa, hakuwa amesogea tumboni bado.

198 Huyu hapa maskini Mariamu anakuja, naye anaingia mbio, naye Elisabeti anavuta mapazia kwenye dirisha dogo la matofali huko juu na kumwona Mariamu akija, kwa hiyo, walikuwa ni binamu, akatoka mbio kumlaki, na kumkumbatia, na kusema, "Loo, Mpenzi, nina furaha sana kukuona."

"Loo, naona, bila shaka, wewe ni mjamzito."

199 "Naam, mimi ni mjamzito." Kasema, "Lakini mimi—mimi nina hofu kidogo," akasema, "ni miezi sita nikiwa na mimba, wala hakuna uhai bado, nami nina wasiwasi kidogo."

Mariamu, huku maskini macho yake yakimetameta, maskini msichana mwenye umri wa miaka kumi na sita au kumi na minane, akasema, "Nitapata Mtoto pia."

"Loo, kwani wewe na Yusufu tayari mmeoana? Nina furaha kusikia hilo."

"Loo, bado, tumechumbiana tu, hatujafunga ndoa bado."

"Ati nawe utampata Mtoto? Kuna shida gani? Vipi kuhusu hili?"

200 Akasema, "Naam, nilikutana na Gabrieli, yule Malaika. Nilikutana na Mungu. Naye akaniambia ya kwamba Kitu hiki kitakatifu kitaitwa Mwana wa Mungu, naye alisema ninapaswa kumwita Jina Lake 'Yesu.'"

201 Na mara tu, mara ya kwanza ambapo Neno hilo *Yesu Kristo* lilipopata kutajwa kwa mdomo wa mwanadamu, maskini huyo mtoto mchanga tumboni mwa—mwa Elisabeti akawa hai, akaanza kuruka na kuruka-ruka kwa furaha. Hiyo ni kweli. Nayo imani yake . . . Kasema alikuwa amejazwa na Roho Mtakatifu, naye akasema, "Ametoka wapi mama wa Bwana wangu? Maana mara sauti ya salamu zako ilipoingia masikioni mwangu, mtoto wangu mchanga aliruka kwa furaha tumboni."

202 Na kama—kama mara ya kwanza ambapo *Yesu Kristo* liliwahi kutajwa kwa mdomo wa mwanadamu lilimfanya mtoto aliyekufa afufuke, linapaswa kufanya nini kwa kanisa linalodai kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu? Amina, katika . . . Kwa nini? Walikuwa wamekutana na Mungu, jambo fulani lilikuwa limetukia.

203 Loo, hakika, ilikuwa ni yule Simoni Petro, mtu huyo alikuwa amefundishwa na baba yake ya kwamba ajapo Masihi, Yeye atakuwa ni nabii. Naye Simoni alikuwa mvuvi, lakini siku moja, wakati alipoenda Uweponi mwa Yesu Kristo, Naye akasema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona, nami nitakuita Petro tangu sasa na kuendelea," alijua Huyo alikuwa ndiye Masihi, alikuwa mtu aliyebadilika tangu siku hiyo na kuendelea, alikuwa anaenda kuvua watu badala ya samaki, kumfanya wavuvi wa watu, kwa sababu alikuwa amekutana na Mungu, alitambua kuwa hilo ni kweli; alikutana Naye.

204 Ilikuwa ni Paulo, Sauli wa Tarso, aliyekuwa akienda zake, wa kidini, aliyefundishwa chini ya Gamalieli, yule mwalimu mashuhuri, alijua mambo yote ya dini ya Kifarisayo kwa undani sana, na kadhalika, alikuwa akishuka kwenda zake, akiwakamata hao watakatifu wote wanaojibingirisha waliokuwa wakifanya hivyo, alikuwa na makaratasi mfukoni mwake kuwakamata wale wote waliokuwa huko Dameski.

205 Na mara ile Nguzo kuu ya Moto ikamzunguka, naye akaanguka kwa miguu yake. Loo, aliamka mtu tofauti. Kwa nini? Alikuwa amekutana na Mungu. Kitu fulani kilikuwa kimembadilisha papo hapo, alipomsikia akisema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Kasema, "U nani Wewe, Bwana?"

Akasema, "Mimi ni Yesu, na ni vigumu kwako kupiga teke michokoo."

206 Kulikuwa na kipofu siku moja, ameketi kando ya barabara akiombaomba, lakini alikutana na Mungu. Alikuwa ameketi pale akiwazia juu ya . . . Mahali maskini kipofu Bartimayo alipokuwa ameketi, alikuwa akiwazia, huko chini mtoni miaka mia kadhaa iliyopita, Yoshua, yule shujaa mkuu, alivuka pamoja na Israeli kule kwenye nchi kavu katika mwezi wa Aprili, wakati Mungu alipochukua mkono Wake wenye nguvu na kuyashikilia hayo maji, "Loo, laiti ningaliishi katika wakati huo, ningalishuka niende kule, na kusema, 'Yoshua, niombee.' Lakini ole wangu, kuhani ananiambia siku za miujiza zimepita.

207 "Loo, wazia tu, moja kwa moja kwenye barabara hii, barabara hii ya mawe mahali nilipo, walikuja Eliya na Elisha, wameshikana mikono, wakishuka kwenda Yordani kuifungua Yordani. Laiti ningalikuwa nikiishi hapa katika siku hiyo, ningalitoka nje na kusema, 'Manabii wa Bwana Mungu, niombeeni.' Lakini ole wangu, siku za miujiza zimepita, kuhani anasema.

208 "Basi wazia, wakati Yoshua alipokuwa akijiandaa kupiga kambi, ama, kuzizingira kuta hizi zinazozunguka Yerusalemu, kwenye moja ya mawe ninayokalia sasa . . . Siku moja alipokuwa huko nje akiangalia huku na huku, akiangalia kuta pande zote, mbona kulitokea . . . Alimwona Mtu amesimama amechomoa upanga Wake. Yoshua, yule shujaa, amiri jeshi mkuu, akauchomoa upanga wake, akamkimbilia, na kusema, 'Uko pamoja nasi? Je, uko pamoja na adui?'

"Akasema, 'Mimi ndimi Amiri wa jeshi la Bwana.' Yoshua akatupa chini upanga wake, akatoa chepeo yake, akasujudu miguuni Pake.

209 "Loo, laiti ningalimwona Jemadari huyo mkuu, ningesema, 'Amiri Mkuu wa jeshi la Bwana, mimi ni kipofu, unirehemu.' Loo, jinsi ambavyo angalifanya hivyo kama ingalikuwa . . . Lakini ole wangu, siku za miujiza zimepita."

210 Jinsi ambavyo hakujua ya kwamba, si yadi mia moja kutoka kwake, alisimama Amiri yule yule wa jeshi la Bwana, kwa kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Akasikia kelele. Ajabu ni kwamba, kila mahali Yeye alipo, kuna kelele zinazoendelea.

211 Watu walisema, "Mnapiga kelele nyingi kupita kiasi." Hapa ndipo mahali panyamavu sana utakapopata kuishi. Ukienda Mbinguni, hata Malaika wanaimba mchana na usiku, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana." Ukienda kuzimu, ni kulia, na kuomboleza, na kusaga meno; hapa ndipo mahali panyamavu sana utakapopata kuishi.

Na hapo, wakati Yesu alipopitia pale, mtu fulani alimsukuma chini na kadhalika, na kumkanyaga, akapita.

212 Nami ninaweza kusikia hilo shirika la wahudumu, wote wamesimama huko nje, kasema, "Aisee, wananiambia wewe ni nabii. Wanasema ati ulimfufua mtu aliyekufa, tuna makaburi

yaliyojaa hao hapa juu. Njoo ukatufufulie mmoja, tutakuamini." Mnaona, Mungu hamfanyii vitimbi mtu yeyote. La, la. Angeweza, lakini kichwa Chake cha thamani kilielekezwa Yerusalemu na Kalvari, akizichukua dhambi za ulimwengu, Yeye akaendelea mbele, huku anatupiwa tunda lililooza na kadhalika.

Ndipo mtu fulani akamsukuma nje moja kwa moja. Ninawazia ilikuwa ni msichana aliyekuja, akasema, "Bwana, kuna nini?"

213 Maskini, ombaomba aliyevaa matambara, akasema, "Mama, mimi ni kipofu. Na kulikuwa na Mtu fulani aliyepita hapa, nao walikuwa wakipigia mayowe jambo moja na lingine. Ilikuwa ni nini?"

"Bwana, mimi ni mmoja wa wanafunzi Wake. Hivi hujawahi kusikia habari za yule Nabii kijana wa Galilaya?"

"La. Nabii yupi kijana?"

214 "Vema, unajua torati yetu inaahidi ya kwamba wakati . . . atakuja, siku moja, Masihi, na Mwana wa Daudi anakuja? Na atakapokuja, mwajua, yule Nabii mkuu . . . "

215 "Loo, huyo ni Yeye? Huo ni Yeye?" Ndipo akasimama (Asingeweza kumsikia kwa kelele hizo zote, maelfu. Na kama ukienda huko Yeriko na kuona mahali alipokuwa ameketi, na mahali Yesu alipokuwa wakati aliposimama, haiwezekani Kwake kumsikia, lakini imani yake ilimsimamisha.) "Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu."

Pamoja na huko kupiga mayowe kote kwa jambo moja, na lingine. Mmoja, "Salamu Nabii! Salamu Mwana wa Mungu!"

Na huyo mwingine akasema, "Mwondoeni huyo laghai, Beelzebuli, mpiga ramli," kadhalika, umati huo wote uliochanganyikana.

216 Lakini imani yake! Nayo Biblia ilisema, "Yesu akasimama kimya." Loo, natumaini kuhubiri kabla sijaondoka hapa juu ya *Yesu Akasimama Kimya*. Loo, jamani! Siku moja wakati utasimama kimya. Ndipo akasimama kimya, imani yake ilimgusa, maskini ombaomba mmoja kipofu. Akageuka, Naye akauliza, akauliza alichotaka. Naye akasema, "Ili nipate kuona."

Akasema, "Imani yako imekuokoa." Haleluya! Tangu wakati huo na kuendelea angeweza kuona. Kwa nini? Alikutana na Mungu.

217 Kulikuwa na mwendawazimu, siku moja, huko Gadara, ambaye alikuwa akijikatakata, nao wangemfunga kwa minyororo, na nguvu zake za mara kumi ya mtu wa kawaida zingeweza kuvunja nguvu za hiyo minyororo. Daima niliwazia, kama alikuwa chini ya ushawishi wa ibilisi kikamilifu hivi . . . Ibilisi anapomshika mtu, mwendawazimu, inahitaji wanaume na wanaume kumshikilia. Yeye huivunja minyororo

hiyo, amejisalimisha kabisa kwa ibilisi. Kama angeweza kuvunja minyororo, ni zaidi sana vipi sisi tungeweza kuivunja, tukijisalimisha kabisa kwa Mungu? Nguvu za Mungu zina nguvu zaidi jinsi gani kuliko za ibilisi?

218 Naye huyo hapo, maskini mwendawazimu huyu, naye daima alikuwa huko nje makaburini, akijikata kwa mawe, na kumshambulia kila mtu. Lakini siku moja alikutana na Mungu, mambo yakambadilikia. Baada ya hapo akavikwa nguo, akiwa na akili timamu. Kwa nini? Alikuwa amekutana na Mungu.

219 Mwenye ukoma alisimama karibu na lango akiomba. Siku moja Yesu wa Nazareti akapitia hapo, naye akasema, "Ukitaka, waweza kunitakasa."

Akasema, "Nataka; takasika." Na tangu wakati huo akatakasika.

220 Kuna maskini mwanamke mzinzi, kama tulivyomzungumzia jana usiku, aliyeingia kisiri langoni, nje ya lango, akatoka nje kwenda kwenye kisima cha mjini kuchota maji siku moja. Ndani ya nafsi yake kulikuwa na Maandiko kwamba Masihi huyo ajapo kile atakachokuwa. Naye alikuwa kahaba, alikuwa mwanamke mbaya sana. Alikuwa na waume, naye akiishi na mmoja wakati huo, pasipo kuolewa naye, kwa hiyo mnajua alikuwa ni mwanamke mwenye sifa mbaya. Ndipo alipomwona Yesu na kumsikia akisema, "Nenda kamwite mumeo."

Alisema, "Sina yeyote."

Kasema, "Ulisema vema. Kwa maana umekuwa na watano; na yule unayeishi naye sasa siye wako."

Akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii. Nasi tunajua ajapo Masihi atatwambia mambo haya."

Yeye alisema nini? Alisema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye."

221 Alikuwa ni mwanamke aliyebadilika. Angalieni, alipoingia mjini...Ni kukiuka maadili kabisa kwa mwanamke wa aina hiyo...ama mwanamume kumsikiliza, lakini alikuwa amekutana na Mungu, ilibidi kitu fulani kimsikilize. Hiyo ni kweli. Alikuwa amekutana na Mungu, ilibidi kitu fulani kisikilize.

222 Wakati mtu anapokutana na Mungu kweli...Nawazia tungeweza kuona baadhi ya hao watu hapa waliokuwa kwenye vitanda hivi vya wagonjwa jana usiku, na kiti cha magurudumu, wameketi hapa, waulizeni leo, wakikutana na Mungu, watabadilishwa tangu wakati huo na kuendelea, jambo fulani lilitukia. Tangu wakati ambapo Mungu ananena, jambo fulani linatukia. Chochote kinachokutana na Mungu, tangu wakati huo na kuendelea kimebadilika.

223 Sasa hebu kidogo. Mauti ilikutana Naye wakati mmoja. Kweli. Sasa, tunafunga. Mauti ilikutana Naye. Mnajua, ibilisi kamwe hakuamini huyo alikuwa ni Mungu. Daima alidhani

ilikuwa ni, ninii tu, nabii fulani wa kawaida. Lakini hakutambua ilikuwa ni nini, hakujua huyo alikuwa ni Imanueli, kwamba Huo ulikuwa ni nyama na mwili wa Mungu, ya kwamba Yeye alifanyika mwili akakaa kwetu.

224 Wakati alipomweka juu ya mlima siku hiyo, alisema, "Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu, geuza mawe haya yawe mkate." Mnaona, ibilisi yuyo huyo wa kale angali hai leo.

225 Walikuwa Naye kule chini uani wakati huo, walijua angeweza kuyatambua mawazo ya watu, kwa hiyo wakaweka kitambaa usoni Mwake, na kuchukua fimbo, na kumpiga kichwani, kasema, "Sasa, kama wewe ni nabii tuambie ni nani aliyekupiga." Kamwe hakufungua kinywa Chake; Yeye hamfanyii ibilisi vitimbi.

Huko juu msalabani, kasema, "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, shuka chini nasi tutakuamini."

Ibilisi yuyo huyo wa kale anaishi ndani ya watu leo, jambo lile lile, "Ukifanya hivyo, hebu nikuone ukifanya *hili*. Hebu nikuone ukifanya *lile*."

Akasema, "Nafanya tu yale Baba anayonionyesha."

226 Kwa hiyo siku moja walipokuwa Naye. . .Hebu tuchukue mchezo mdogo wa kuigiza tunapofunga. Ni siku ya kutisha, jua linaonekana la kiajabu, hakujawahi kuwa na siku kama hiyo, kamwe hakutakuwako. Loo, ni jambo la kutisha sana! Deni kutoka Edeni halina budi kulipwa. Siku ya kutisha sana! Nasi tunaanza kuona asubuhi na mapema, tumesimama ghorofani, nasikia kelele. Hebu twende tukainue pazia na tuangalie. Nasikia kitu fulani kikishuka kuja barabarani, "Bump, bump, bump." Ni kitu gani? Ni msalaba wa kale unaoparuza.

227 Ninamwona maskini mwanamke mmoja akikimbia mbele yao, akisema, "Kwani amefanya nini? Amefanya nini ila kuihubiri Injili? Amefanya nini ila kuwaponya wagonjwa?"

Ninaona mkono mgumu ukimpiga kofi mdomoni na kusema, "Kaa chini. Hivi ninyi watu mngemwamini mwanamke huyo, kahaba, kabla hamjamwamini kuhani wenu?"

Asingeweza kunena amani yake. Ilibidi wakati wake ufike kwa ajili ya kitu kingine, msalaba ukikokotwa.

228 Alikuwa na joho mabegani Mwake, anapoanza kupanda kilima, ninaona madoa madogo mekundu kote kwenye koti Lake. Sijui ni nini. Maskini mwili Wake dhaifu, taji ya miiba kichwani Mwake, mate ya dhihaka yakining'inia kote usoni Mwake, alikuwa amefanya nini kustahili hayo? Hiyo ndiyo adhabu anayolipa kwa ajili yangu, kwa ajili yako.

229 Angalieni hayo madoa madogo, hebu na tuyaangalie kwa dakika moja. Anapopanda akijikokota, maskini mwili Wake ni dhaifu, nao wanampiga mijeledi, na kumfanya aendelee mbele, Naye anaukokota maskini msalaba huu mkubwa juu ya kilima.

Baada ya kitambo kidogo naona madoa haya yote madogo-madogo yakianza kuwa makubwa zaidi, makubwa zaidi, baada ya kitambo kidogo yote yanakuwa tone moja kubwa, ninalisikia likirashia mguuni Mwake. Anashuka. Anazidi kuwa mnyonge zaidi na zaidi.

Ninaweza kuona kila kitu. Wanafunzi Wake wameondoka, ni nani anayesimama karibu Naye? Hakuna mtu, ameachwa na Mungu na mwanadamu. Huyu hapa anapanda kilima.

230 Ndipo ninaona mauti ikija na kusema, "Uh-huh. Nimempata. Nilithibitisha ya kwamba Yeye si Mungu. Nilimjaribu. Nilitoka huko nje. . . Kama angalikuwa ni Mungu, angaligeuza hayo mawe yakawa mkate. Angewezaje kusimama pale, katika uga huo, akawaacha hao askari wamtemee mate usoni, na kumfunga kitambaa usoni Mwake, na kumwambia aseme ni nani aliyempiga? Mbona, kama angalikuwa ni Mungu, angalijua hilo. Ninajua Yeye si Mungu." Kamwe hakuliamini.

231 Naye anapopanda kilima, ninamwona huyo nyuki wa mauti akitokea, anaanza kuvuma karibu Naye, anamchoma. . . kumchoma, akivumisha kote kumzunguka. Muda si muda mwajua, anaanza kushangaa. Ilikuwa ni kitu gani? Mauti ilikuwa inazunguka, mvumaji, kama mdudu, nyuki.

232 Lakini mnajua nini? Kama nyuki akiwahi kuuchomelea mwiba wake ndani, yeye huung'oa mwiba wake. Hawezi kuuma tena. Alikuwa ameuchomelea katika manabii wengi, alikuwa ameuchomelea katika watu wengi wenye haki, lakini wakati huo, alipouchomelea kwa Mungu, aliung'oa mwiba wake. Mauti yakapoteza mwiba wake.

233 Si ajabu mtu aliyekuja baadaye, alisema, "Ewe mauti, u wapi mwiba wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Mungu ashukuriwe. . . " Wakati alipouchomelea mwiba huo wa mauti mwilini mwa Imanueli, huo mwiba uling'olewa.

234 Na leo hii tunaweza kutembea mbele ya mauti, na nyuki anaweza kuvuma na kupiga kelele, lakini kamwe haitatuogopesha. La, bwana. Hana mwiba, huo mwiba umeondolewa. Kwa nini? Mauti ilikutana na Mungu. Na ilipokutana na Mungu, iliung'oa huo mwiba wa mauti. Nina furaha kukutana Naye. Hivi hamna furaha? Na tuombe.

235 Baba wa Mbinguni, ninapowazia juu ya Damu hiyo inayomwagika kutoka kwenye mishipa ya Imanueli, ule msalaba wa kale unaoparuza ukikokota nyayo za miguu ya mwenye kuubeba akielekea Kalvari. . . Shetani, akiona maskini dhihaka hizo za kale, mate ya midomoni yakining'inia usoni Mwake, alisema, "Huyo hawezi kuwa Mungu, Huyo hawezi kuwa Imanueli, kwa hiyo nitadunga mwiba wangu ndani Yake. Nitampata hivi karibuni sana."

236 Lakini loo, jinsi alivyoshindwa wakati huo! Wakati mwiba wa mauti ulipomgusa Mungu, ilipoteza mwiba wake. Nina

furaha sana leo, Bwana, nikijua pia, ya kwamba sina budi kushuka kwenye barabara hiyo, lakini mauti itapoteza... imekwisha kupoteza mwiba wake.

237 Niko huru usiku wa leo. Haleluya! Nina furaha sana kwamba niko huru. Uchungu wa mauti umekwisha. Kifo kinaweza kuja na kuvuma, kinaweza kuja na kunitisha, kinaweza kuja kunivuta niondoke, lakini kama vile mwandishi mmoja alivyosema, "Mungu alikifunga kwenye mkokoteni, kinaweza tu kunivuta nifike Mbele Zake mahali ninapotamani kuwa," ambapo kila mwaminio anatamani kuwa.

Kwa hiyo mauti haina mwiba, imekuwa ni ushindi, "Mungu ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Yesu Kristo."

238 Wakati tumeinamisha vichwa vyetu, kila mtu katika maombi, ni wangapi hapa ndani ambao...wanajua kama mlikuwa mkifa usiku wa leo kwamba kamwe hujawahi kuwasiliana na Mungu dhahiri sana hata ungeweza kuchukua kila Neno kuwa ni Neno Lake, na kwamba unatii kila Neno, na unajua ya kwamba kama unafanya makosa, unajua ya kwamba mauti ingekuwa na mwiba kwako, maana ungeshangaa kama kweli ungeokoka au la?

239 Sitawaita huku juu, madhabahuni, nitawaulizeni tu mahali mlipo. Ukipenda, na kuamini, usiku wa leo, ya kwamba Mungu atakutolea mwiba huo wa mauti, kupitia kwa Yesu Kristo, nawe unataka kulikubali hivyo, inua mkono wako, useme, "Ninataka kukutana na Mungu."

240 Mungu akubariki huko nyuma, Jamani Mwanangu. Mungu awabariki. Mungu awabariki, huko juu kwenye roshani. Mungu awabariki hapa chini. Huko juu kwenye roshani? Mungu akubariki, Kijana Mwanamume. Mungu awabariki huko nyuma kabisa. Anaiona mikono yenu. Kila mtu akiomba. Huo ni wito wa madhabahuni. Mungu akubariki, unayeketi hapa, Bwana. Huenda umefanya mambo mengi mazuri maishani, lakini hilo ndilo jambo kuu sana ulilowahi kufanya.

241 Kumbuka, ulipoinua mkono wako ulivunja kila kanuni ya kisayansi. Sayansi inasema kwamba nguvu za uvutano hazina budi kushikilia mkono wako chini, lakini uliinua mkono wako, ikionyesha ya kwamba kuna nguvu ndani yako kufanya uamuzi. Na kwamba ulifanya hivyo, uliinua mkono wako, maanisha hilo kutoka moyoni mwako, na jambo fulani litatendeka.

242 Mtu mwingine inua mkono wako, useme, "Unikumbuke." Mungu akubariki, Dada. Mungu akubariki, Dada. Mungu akubariki, Ndugu. Mungu akubariki. Hilo ni jema. Huko juu kwenye roshani tena, hebu tupande huko juu kabisa. Ni wangapi huko juu? Loo, nafsi, mshiriki wa kanisa asiyemjua Mungu... Mungu akubariki, ewe mtu mdogo hapa mbele.

243 Mtu mwingine? Inua mkono wako, useme, "Loo, yote nijuayo, mimi ni mfuasi wa kanisa. Yote nijuayo, nimepaza sauti.

Yote nijuayo, nilinena kwa lugha.” Loo, ndugu, nimewasikia pepo wakicheza katika roho, na kunena kwa lugha, na kupaza sauti, na hilo—hilo halininii . . . “Kwa matunda yao mtawatambua.” Bila shaka.

244 Mvua hunyea ngano na magugu pamoja. Bila shaka. Yote mawili huifurahia mvua, hiyo ni kweli, inayafurahisha yote mawili. Nayo hunyea moja kwa moja katika kundi juu ya mnafiki na juu ya Mkristo, pia. Lakini kama maisha yako hayaambatani na Biblia ya Mungu, basi afadhali uinue mkono wako na kusema, “Mungu, unirehemu, na unifanye kile ninachopaswa kuwa. Neema Yake inaweza kunifanya kile ninachopaswa kuwa.” Mungu akubariki, Kijana Mwanamume. Mungu akubariki, Mama. Hilo ni zuri. Mungu awabariki.

245 Sitaki kuudhi hisia zenu, lakini ninyi wanawake mnawezaje kuketi hapa na kujua ya kwamba Biblia inawaambia kwamba hata ni makosa kwenu kukata nywele zenu, kwamba unamvunjia mume wako heshima unapofanya hivyo? Unajithibitisha kama mwanamke wa mtaani unapofanya jambo kama hilo. Na kwa sababu ya Malaika, unapaswa kuwa na nywele ndefu. Malaika gani? Malaika wa agano, Malaika, mjumbe wa siku hii, Malaika wa saba, ambaye anapiga baragumu leo. Basi bado unajua ya kwamba umekosea? Huenda Adamu wako amekuacha uendelee na kutenda mabaya, Hawa, na kusema haileti tofauti. Hakika inaleta tofauti. Usininii . . . Kila amri ya Mungu ni ya kweli. Hawa aligeuza tu ninii yake . . . aligeuka tu kwa dakika moja. Kama umekosea, kubali umekosea. Maisha yako mwenyewe yanathibitisha ya kwamba umekosea.

246 Mtu fulani alinifuata, si muda mrefu uliopita, kasema, “Ndugu Branham, kwa nini unasema hivyo kwa hao wanawake, kuhusu mavazi yao?” Mtu mashuhuri, akasema, “Nitakuwekea mikono, na kukuombea.”

Nikasema, “Kama utaniruhusu nikuwekee mikono na kukuombea.” Nikasema, “Sikiliza . . . ”

Akasema, “Kwa nini usiachane na hao wanawake? Watu wanakuchukulia kama nabii.”

Nikasema, “Mimi si nabii.”

Akasema, “Watu wanakuchukulia hivyo. Kwa nini usiwafundishe jinsi ya kupata karama kuu za kiroho na kadhalika?”

247 Nikasema, “Kama hawana adabu ya kawaida ya kujifunza ABC zao, wanawezaje . . . watajuaje, watajuaje jinsi ya kujifunza aljebra, kama hata hawachukui ABC zao?” *ABC* ni “Sikuzote Mwamini Kristo.” [Kiingereza: Always Believe Christ—Mf.]

248 Lichukue Neno Lake kwanza, acha liwe la kwanza maishani mwako. Kama huwezi kufanya hivyo, utajifunzaje jambo lingine

lolote? Kanisa la Kipentekoste litawezaje kuinuka juu ya mambo lijuayo, hayo yatakuwa njiani mwako maadamu ungali hai? Sasa, litie hili alama na uone kama halifanyiki.

249 Kumbuka, kama hilo halikusumbui maadamu ungali hai . . . Na kama dhambi moja ilimshikilia Hawa, ama, ilifanya haya yote . . . Kila ugonjwa, mauti, na huzuni ilitokana na mwanamke mmoja akihoji tu kwamba ilikuwa ni sawa.

250 Ni majaliwa yako ya Marekani, mnasema. Loo, naam. Kama wewe ni mwana-kondoo, mwana-kondoo hupoteza haki zake; yeye hana ila kitu kimoja, sufu, naye hupoteza hiyo. Kama wewe ni mwana-kondoo utapoteza haki zako za Marekani, kumtumikia Mungu.

Useme, "Ninaweza kuvaa nitakavyo, si kazi yako."

251 Si mimi, ndugu, dada, ni Biblia. Mungu alimwumba mwanamume, na kumfanya avae kama mwanamume, akamfanya mwanamke kuvaa kama mwanamke, akawafanya watende tofauti, kisha akafanya maagano mawili pamoja nao, na kadhalika; imekuwa hivyo daima.

252 Nuru imekuja. Huenda Adamu wako akakuacha upite nayo, lakini, ndugu, Mungu hatakuacha, maana hilo ni Neno Lake. Sasa, ninyi wanaume mnaoketi huku na kufanya mambo kama hayo: Hivi hamwoni aibu, ndugu, mashemasi? Watu wanaosema wao ni watu wa Mungu wanatenda hivyo, wakati hilo—hilo ndilo somo lake la kwanza kabisa. Unawezaje kuingia katika mambo yenye kilindi ya kumpambanua Roho na mambo kama hayo, kama hata huchukui mambo ya kwanza?

253 Kutana na Mungu, uone kuna tofauti gani. Angalia tofauti. Itakufanya utende mema, itakufanyia jambo fulani, itakubadilisha. Sasa, Biblia inasema hivyo.

254 Ninyi wanawake msingejipodoa kwa rangi ya makucha, ama vipodozi, vyovyote mnavyoviita, bure. Biblia haisemi neno juu ya jambo hilo. Lakini angalieni yale mnayofanya sasa, jambo ambalo Biblia *inasema* lisifanywe. Unaona?

255 Ninyi, labda, ninyi wanaume kamwe hamngelewa kwa sababu yoyote duniani, kisha mwe na wake wawili au watatu mbalimbali walio hai, mwe shemasi kanisani.

Kuwaongoa watu, "Mwazunguka bahari," Yesu alisema, "kumfanya mwongofu mmoja . . ."

256 Mnasema, "Hiyo ni njia mbaya sana ya kufanya wito wa madhabahuni." Ndugu, kama watu hawaji kwa Neno la Mungu, hadithi hizi za kuhuzunisha ni za nini? Huna budi kuja ukitambua ya kwamba umekosea.

257 Sasa, uko tayari, chini ya nguvu za Mungu, chini ya hukumu yako mwenyewe, kusema ya kwamba "Nimekosea, ninainua mkono wangu. Nimeangalia maisha yangu mwenyewe na kuona ya kwamba nimekosea. Mimi ni mfuasi wa kanisa,

ninaenda kanisani, ninajaribu kuwa mwaminifu, lakini naona nimefanya . . . nilikosa shabaha. Niko tayari kujisalimisha na—na kusema kwamba ninarudi kwenye misingi ya Biblia ya kitu hiki. Ninainua mkono wangu"? Inua mkono wako.

258 Mungu akubariki, Bwana. Hilo linahitaji adabu. Mungu akubariki, Mama. Mungu akubariki. Mungu akubariki, Bwana. Hiyo inahitaji wanaume halisi. Mtu mwingine? Mungu akubariki, ndugu yangu. Hiyo ni kweli. Mungu akubariki. Kuna angalau watu mia tatu hapa, wanaopaswa kufanya hivyo. Hilo linawahitaji wengi sana, lakini . . . Mungu akubariki, Bwana, huo ni uaminifu.

259 Sema, "Ninafanya tu uamuzi wangu. Ninasema sasa hivi, 'Tangu sasa na kuendelea, Mungu, nitapigwa chapa ndani na nje. Nitakuwa Mkristo halisi. Nitaliamini Neno hili lote." Ama, "Sitaamini lolote. Ninarudi ulimwenguni." Ungekuwa bora zaidi. Hiyo ni kweli.

260 Huwezi kuwatofautisha Wakristo na hao wengine. Wote, karibu wanafanana. Kile kinachodhaniwa kuwa ni Kanisa kinakuwa katika hali mbaya sana. Hima. Mungu hana budi kumwandaa Bibi-arusi, hasa, akimfanya tayari. "Saa ya . . . imekuja, naye Bibi-arusi amejifanya Mwenyewe tayari." Uko tayari? Uko tayari? Ninauliza mara nyingine tena, katika Jina la Yesu: Uko tayari? Asante, Bwana. Mungu akubariki.

261 Baba yetu wa Mbinguni, hawa ambao wameinua mikono yao, yapata dazani mbili au zaidi, jalia wawe na amani. Jalia wajue ya kwamba Wewe uko tayari kuvuta hatia yote ya mwiba kutoka kwake, na kuwaweka huru, usiku wa leo, kwa Roho Mtakatifu. Mungu, yabariki makanisa haya.

262 Hili hapa kundi zuri la watu, Mungu. Wameketi hapa kwa muda mrefu sana, wakisikiliza, wakingojea, basi kwa nini Shetani anakuja moja kwa moja huku na kuzitia giza akili zao, mara tu wakati unapowadia kwao kukubali? Nawe umejithibitisha Mwenyewe dhahiri sana hapa. Inawezekanaje?

263 Lakini Mungu, jalia damu ya mtu yeyote isiwe mikononi mwangu; niko huru. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawajalia hawa rehema ya Mungu. Ninawakabidhi Kwako kama Mzao mwaminifu ambaye nuru ya Mungu imemwangazia. Uzima ulipiga upesi, nao wakainua mikono yao, na kusema, "Nimekosea, ninatambua jambo hilo, niko tayari kufanya mema. Nimekosea, nami niko tayari kutengeneza njia zangu sasa hivi, na kumjia Mungu." Jalia, Baba, ya kwamba watakua wafikie vimo vikubwa vya Wakristo.

264 Tunasikia usiku wa leo, kuhusu maamuzi *mengi sana*. Mawe yanafaa nini bila mwashi? Watu wanataka wafuasi zaidi kanisani mwao, "Je, utafanya uamuzi?" Kufingirisha jiwe, huko ni kukiri. Bila shaka. Lakini jiwe hilo linafaa nini, kama hakuna mwashi pale aliye na Neno kali la Mungu lenye makali kuwili

kulichonga likawa mwana ama binti wa Mungu, kulifanya litoshee ndani ya hilo jengo? Tunahitaji waashi, wachonga mawe kwa Neno la Mungu, kuyakata maungamo yawe nguzo halisi za Kanisa la Mungu. Tujalie, Bwana.

265 Jalia kisu kikali cha Mungu kitahiri ulimwengu wote umwondokee kila mmoja wetu, na kutufanya viumbe vipya katika Kristo Yesu. Saa inakuja. Watu hawajui kwamba saa hizi zimewadia, mambo makuu yanaendelea. Na sasa, watu wameninii, kama tu watu wa kale, Bwana, waliwapita, wala hawakujua.

266 Jalia kwamba kila mmoja wa hawa aokolewe. Jalia wapate baadhi ya makanisa haya mazuri, hapa, wahudumu hawa. Labda, kama wao ni wa moja la hayo, na wamwendee mchungaji wao, na kusema, "Mchungaji, nimekuwa makosani, Ninayanyosha maisha yangu. Ninakuja sasa kuwa mfuasi halisi wa kanisa lako, naja sasa kuwa nuru. Sitapuliza sana kutoka kwa hiyo filimbi, bali nitaifanyiza kazi. Ninaenda nyumba hadi nyumba, mahali mahali, nitawaleta wengine katika ushirika huu mkuu wa Kristo. Nitaenda pembeni mwa barabara, nitasambaza vitini, nitafanya chochote niwezacho kufanya.

267 "Nitazungumza na jirani yangu, mtu wangu wa maziwa, mvulana wangu wa gazeti, kila mtu niwezaye, nitazungumza nao katika upendo mtamu, wa Roho Mtakatifu. Nitakolea chumvi sana, hata nitawafanya waone kiu kuwa kama mimi." Mungu, tujalie. Loo, si kama walimwengu wengine, bali ni kuwa tofauti, kubadilishwa, kufanywa kama binti za Mungu, wana wa Mungu. Tujalie.

Ninawakabidhi Kwako katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Sasa, Mungu wa Mbinguni na awaangalie.

268 Wakati mmoja . . . Ninataka kuwasimulia hadithi ndogo kabla ya kuondoka, maana ilinibidi kukata sana. Huko kusini, walikuwa wakiuza watumwa. Nao wangekuja na kuwanunua kama tu vile unavyonunua gari la mtumba uwanjani, unapata hati ya mauzo kwa ajili yake, kama tu vile ungefanya, ya wanadamu, kamwe haikuwa sahihi. Mungu kamwe hakukusudia wanadamu wawe watumwa.

Na kungekuwa na madalali waliopitia hapo, na kununua watumwa wakubwa wenye afya, na kuwazalisha na wanawake wazito zaidi, na mambo kama hayo, kufanya watumwa bora zaidi.

269 Wakati mmoja, kulikuwa na shamba kubwa, niliambiwa, kwamba walikuwa na watumwa wengi, ndipo dalali mmoja akaja, akasema, "Ningetaka kuwaangalia watumwa wako."

Kasema, "Nina yapata mia moja hapa, waangalie."

270 Naye akawaona wote. Walikuwa na huzuni. Walikuwa wametolewa Afrika, kamwe hawangerudi tena. Waliwapiga

mijeledi na kuwalazimisha wafanye kazi, kwa sababu hawakutaka kufanya kazi. Walikuwa na huzuni, walikuwa mbali na baba, mama, mume, watoto wachanga, na kadhalika, kamwe hawangewaona tena. Walikuwa katika nchi ya kigeni, kamwe hawangewaona wapendwa wao tena.

271 Lakini ilitokea walimwona kijana mmoja pale, jamani, alikuwa kifua mbele, kidevu juu, haikuwalazimu kumcharaza mijeledi, alikuwa chonjo kila wakati. Huyo dalali akasema, "Ningetaka kumnunua *huyo* mtumwa."

Akasema, "Hauzwi."

Akasema, "Ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana?" Kasema, "Kwani yeye ndiye bosi wa hao wengine?"

Kasema, "La, yeye ni mtumwa tu."

Akasema, "Labda unamlisha vizuri kuliko unavyowalisha hao wengine?"

Kasema, "La. Yeye hula huko nje manchani pamoja na hao wengine, yeye ni mtumwa tu."

Kasema, "Ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana na hao wengine?"

272 Kasema, "Wakati mmoja mimi mwenyewe nilishangaa, lakini nikaja kugundua ya kwamba katika nchi ya uenyeji wake baba yake ndiye chifu, mfalme wa kabila hilo. Naye anajua ya kwamba yeye ni mwana wa mfalme, anajitendekeza kama mmoja."

273 Marafiki, tuko katika ulimwengu wenye dhambi. Enyi wanawake, ninyi ni binti za Mfalme; ndugu, ninyi ni wana wa Mfalme, hebu na tuenende kama wana na binti za Mfalme, moja kwa moja katika ulimwengu huu. Msiwe kama wao, kuwaiga, sisi ni tofauti. Tunakuja. . .Tunatoka ninii nyingine. . .Sisi ni wageni hapa, sisi ni wasafiri. Hebu na tujiendeleze, tutende tofauti, tuwe tofauti, tuwe kama huko juu Mbinguni.

274 Siku chache zilizopita mimi na mke wangu, kabla hatujaja huku, tulienda kwenye supamaketi, tukamwona mwanamke aliyekuwa amevaa gauni. Meda akasema, "Si ni ajabu hiyo, huyo mama?" Akasema, "Billy, nataka kukuuliza," kasema, "Ninawajua baadhi ya hao wanawake, wanaimba katika kwaya hapa katika makanisa haya ya kimadhehebu," kasema, "mbona watu wetu. . .?"

275 Nikasema, "Mpenzi, angalia, angalia, sisi si wa ulimwengu. Unaona, ninapoenda Ujerumani, Ujerumani ina mtindo wake; nikienda Ufini, ina mtindo wake; nikienda kwa mataifa mengine, wana mtindo wao." Kisha nikasema, "Marekani, ina mtindo wake."

Lakini nikasema. . .Akasema, "Vema, hivi sisi si Wamarekani?"

276 Nikasema, "La, mpenzi, sisi si Wamarekani, sisi ni Wakristo. Tunaishi hapa, bila shaka, kama taifa, *hili* ndilo letu." Lakini nikasema, "Sisi tumetoka Juu, basi wanawake wetu hawana budi kutenda kama Huko juu. Hatuna budi kutenda kama Kule juu, hiyo ndiyo sababu hatutendi kama watu wa ulimwengu, sisi ni tofauti."

277 Tunapaswa kuwa, enyi marafiki, tunapaswa kuwa tofauti. Mnajua hilo. Simaanishi kuwaudhi, wala simaanishi kuudhi hisia zenu, ninamaanisha tu kuwa mwaminifu kama mtumishi wa Kristo.

278 Huwezi kucheza-cheza. Huwezi kuwa ki—ki—ki—ki—kibaraka cha umma, na halafu uwe mtumishi wa Mungu. Inakubidi ama kuwa mwaminifu kwa Mungu, au—au uwauzie wa—watu haki zako za mzaliwa wa kwanza. Na yangu haiuzwi, na ninajua yako haiuzwi pia.

Kwa hiyo hebu tulihubiri Neno, tuliamini Neno, tusimame kwenye Neno, tuishi kwa Neno, hiyo ni kweli, na tuwe Wakristo halisi.

279 Roho Mtakatifu yupo hapa. Mnaamini hilo? Ni wangapi wenu walio na kadi za maombi? Inueni mikono yenu. Tumechelewa sana kuwa na mstari wa maombi. Ninyi msio na kadi za maombi mlio wagonjwa, mnaohitaji kitu fulani, inueni mikono yenu, msio na kadi za maombi. Aminini. Sasa, ninyi aminini.

280 Sasa, angalieni hapa. Sasa, kama ikitokea nimwite mtu aliye na kadi ya maombi, ninawatakeni mniambie hivyo, maana mtaingia kwenye mstari wa maombi, hawa wasio na kadi za maombi hawataingia. Ninataka uchaji wenu dakika mbili tu, dakika tatu.

281 Yote ambayo ningesema hayangemaanisha chochote, Neno moja kutoka Kwake lingemaanisha zaidi ya yote ambayo ningeweza kusema katika miaka milioni moja, Neno moja kutoka Kwake.

282 Sasa, je, mnaamini yale ninayohubiri ni kweli, kuhusu watu kuirudia Biblia, kumrudia Mungu, nalo Neno limefanyika mwili ndani yetu, likikaa miongoni mwetu hapa, nalo Kanisa linajiandaa Lenyewe na kupokea, sasa, ishara Yake ya mwisho?

283 Tumekuwa na miujiza na ishara, na kunena kwa lugha, na "Kupanda juu, kupita kote kote," lakini mnakumbuka, Biblia ilisema, nabii alisema, "Kutakuwako na siku ambayo haitaitwa mchana wala usiku. Lakini wakati wa jioni kutakuwako nuru." Ni wangapi wanaojua Andiko hilo? Hakika. Vema. Angalieni.

284 Ustaarabu umekuja kutoka mashariki na kulifuata jua magharibi. Hiyo ni kweli? Uko kwenye Pwani ya Magharibi sasa, ukipiga hatua nyingine, unarudi mashariki tena. Ningependa

kuhubiri juu ya jambo hilo: *Wakati Mashariki Na Magharibi Zitakapokutana*. Angalieni.

285 J-u-a hupambazukia mashariki, nalo husafiri kwenye upeo wa macho, na kutua magharibi; jua lile lile linalochomoza mashariki hutua magharibi. Hiyo ni kweli?

286 Sasa, nabii alisema kutakuwako na siku ambayo isingeweza kuitwa mchana wala usiku; ni siku yenye utusitusi, siku yenye ukungu. Tumekuwa na siku ya jambo hilo. Mwanadamu amejua ya kutosha kujiunga na kanisa, kumkubali Kristo kama Mwokozi, kisha kujiunga na dhehebu, hiyo ni Nuru tu kama aliyokuwa nayo.

287 Lakini kumbukeni, ni wakati wa jioni sasa. Ustaarabu uko kwenye Pwani ya Magharibi, naye Mwana yeye yule, M-w-a-n-a, aliyeangazia mashariki, hapo mwanzo, sasa anaangaza magharibi mwishoni. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Mnaona? "Itakuwa nuru wakati wa jioni," Kristo akija, akilikamilisha Kanisa Lake.

288 Ni wangapi wanaojua kuna tofauti kati ya kuonekana kwa Kristo na Kuja kwa Kristo? Ni maneno mawili tofauti. Sasa ni kule kuonekana, kule Kuja kutatukia hivi karibuni. Yeye anaonekana miongoni mwetu, akifanya kazi alizofanya wakati mmoja, Kanisani Mwake. Sasa, wewe ni sehemu ya Kanisa hilo, na kwa neema unaamini; mimi ni mshiriki wa Kanisa hilo.

289 Sasa, mimi si mhubiri, mnajua mimi siye, sina elimu ya kufanya hivyo. Wakati mwingine ninasitasita kusimama hapa karibu na watu wa Mungu, walioitwa kwenye ofisi hiyo. Kunao mitume, manabii, waalimu, wachungaji, na wainjilisti. Si wote mitume, si wote manabii, si wote waalimu, si wote wainjilisti.

290 Ninaposimama hapa. . .Lakini huduma yangu ni huduma tofauti na ya mchungaji ama mwalimu, si—sivyo nilivyo. Na kama mimi ni. . .nikisema mambo vibaya, ndugu, samahani, sikusudii hivyo. Lakini hii ndiyo huduma yangu, mnaona, kumtangaza Yeye, ya kwamba Yeye yupo hapa.

291 Sasa, baadhi yenu hapa. . .Kama karama ya Roho Mtakatifu, ni kitu fulani tu, siwezi kujilegeza, ni kama tu kuingiza gia, lakini Yeye anapofanya hivyo, basi kila roho inatiishwa. Nami ninaangalia, nami ninaweza tu kusema kile ninachoona. Naye msomaji yeyote wa Biblia anajua ya kwamba hilo ndilo lililoahidiwa hasa, na likaja katika Kristo, na kuahidiwa katika siku za mwisho, na yote tuliyosema kulihusu. Na, loo jamani, nina kanda mia tano *na kitu* za mahubiri mbalimbali juu yake, mnaona, kugusia tu ukingo wake hapa, bali ni kweli.

292 Haidhuru uko wapi, amini, na umruhusu anene; na kama nikizungumza, naweza kusema vibaya, maana mimi ni mwanadamu, lakini kama Mungu akija huku, na kuthibitisha yale niliyosema, basi hiyo ni kweli.

293 Mungu alisema, "Akiwepo nabii miongoni mwenu, na kama akisema. . .asemayo yakitimia, basi myasikie," maana Neno la Bwana liliwajia manabii, "na kama ninii yao. . .na kama hayatimii, basi msiyaamini."

294 Sasa, kama nikija hapa na kusema, "Sasa, nitawaponya," basi nimedanganya papo hapo, kwa sababu mmeponywa kila mmoja, kama wewe ni mgonjwa, chochote kile, ama wenye dhambi, ama chochote ulicho, tayari umesamehewa, tayari umeponywa. Kama Yesu angekuwa amesimama hapa amevaa suti hii aliyonipa, asingeweza kukuponya wala kukuokoa, tayari amefanya hivyo. Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? Pale Kalvari gharama ililipwa. Wewe amini tu.

295 Mtu fulani, sasa nitaita tu, kwa namna fulani katika sehemu, mtu fulani huku asiye na kadi ya maombi, omba tu, useme, "Bwana Mungu, siwezi kuamini ya kwamba mtu huyo anayesimama pale, ananiambia uongo. Nimesoma Biblia, nami ninajua anayosema ni kweli. Ni vigumu sana kwangu kulipokea, Bwana, lakini kwa kweli, ninaamini, na—naamini, basi unisaidie sasa.

296 "Naye anasema kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu, nami nina udhaifu." Ama—ama mtu fulani, "Mimi. . .Mume wangu anayeketi hapa." "Mke wangu. . ."

297 Niliona jana usiku, wakati mume mmoja anapoamka kutoka kitandani, mke angemkimbilia; mke anaondoka, mume. . . Nikawaona huko nje uani wakimsifu Mungu. Jinsi ilivyokuwa tamu! Mnaona, mnaona? Kumwombea mtu fulani!

298 Sema, "Ninaomba, Bwana Mungu. Nisaidie kujua, nisaidie. Jalia niguse vazi Lako. Ndipo kama mtu huyo. . .Mtu huyo hanijui, wala mimi simjui, kama akijibu, na kuniambia, kama ulivyofanya katika siku hizo, ukawaambia watu, basi ninajua ya kwamba Wewe u hai, si huyo mhubiri, ni Wewe."

Sasa, tafadhalini, kwa dakika mbili ama tatu tu nyamazeni na muombe. Kaeni kimya, msisogee, ombeni tu.

299 Sasa, kuna mwanamke, yeye ni. . .Unaweza kuinua kichwa chako, ukitaka. Na kama utaangalia, mwangalie aliyesimama papa hapa, moja kwa moja ndani ya njia hii ndogo ya ukumbi, je, unaona ile Nuru ya manjano, inayoonekana ya kaharabu ikizungukazunguka? Iko moja kwa moja juu ya mwanamke. Huyo hapo, moja kwa moja kupitia mlangoni. Sasa, inamkaribia, karibu naye. Ametambua. Alikuwa akiomba. Inakaribia.

300 Huyo mwanamke, hakika wakati huu, anaweza kutambua ya kwamba jambo fulani linaendelea. Anamwombea mpendwa, jamaa aliye na kansa, pia mama, naye huyo mama ana ugonjwa wa moyo. Anatambua sasa Roho Mtakatifu yuko karibu naye. Hata hatoki hapa, yeye hata si Mmarekani, yeye ni Mkanada. Je, una kadi ya maombi? Huna. Hatufahamiani kabisa. Hiyo ni

kweli? Lakini ulikuwa umesimama hapo ukiomba, na mara kitu fulani kitamu sana kikaanza kutukia, kama Kitu fulani kikija juu yako. Hiyo ni kweli? Basi yaliyosemwa ni kweli? Inua mkono wako, kama hayo yote ni kweli.

Sasa, nendeni mkammwulize huyo mwanamke.

Sasa, dada, imeondoka karibu nawe. Ninatumaini ya kwamba umepata ulichoomba. Chochote kilichokuwa, Mungu na akujalie.

301 Sasa, nataka kuwaulizeni jambo fulani. Jinsi . . . Liwazieni tu. Huo hapo mwujiza mkamilifu. Huyo hapo mwanamke, sijawahi kumwona maishani mwangu, hajawahi kuniona, hatufahamiani, na hapa Roho Mtakatifu anashuka, naye anamgusa Yesu Kristo, na kwa karama ya Kiungu, akisimama hapo, ama, akiketi hapo akiomba, ndipo inakuja moja kwa moja na kumfunulia kabisa. Hiyo hapo. Yuko futi thelathini ama arobaini kutoka kwangu, asingeweza kunigusa mimi, alimgusa Yeye.

302 Mtu fulani huku aamini, asiye na kadi ya maombi. Wewe usiye na kadi ya maombi, inua mkono wako ili nipate . . . Ninyi msio na kadi ya maombi, inueni mikono yenu. Baadhi yenu katika hizi machela hapa, ama chochote kile, inua mkono wako. Vema.

303 Hebu na tumwangalie mtu huyu hapa. Huna kadi ya maombi, Bwana. Wewe ni mgeni kwangu, sikujui. Unafikiri nini kuhusu yale niliyohubiri? Unamwamini Kristo Mwana wa Mungu? Unaamini Yeye yuko? Sasa, wewe ukiwa mtu ambaye sijawahi kukutana naye hapo kabla maishani mwangu, lakini unaamini ya kwamba—ya kwamba wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, Yeye (Biblia ilisema ya kwamba Neno ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na hata Huyatambua mawazo ya moyo.) angeweza kujua kuna shida gani?

304 Kama Roho Mtakatifu anaweza kuniambia jambo fulani kukuhusu, wewe ni mtu tu ambaye umeketi chini hapo, na anaweza kuniambia jambo fulani kukuhusu, kile unachotaka, shida yako, jambo fulani ambalo umefanya ama kitu kama hicho, ungejua itabidi litoke kwenye mamlaka fulani mahali fulani, sivyo? Ungeamini kuwa ni Kristo? Ungeamini. Je, ungekubali jambo hilo? Huna budi la sivyo utakufa, kwa sababu umetiwa uvuli wa mauti, ni kansa.

305 Lakini kama utaamini kwa moyo wako wote, kwa yote yaliyo ndani yako, kwa sababu huwezi kuishi, huwezi kurudi, daktari hawezi kukusaidia sasa, umepita hayo, lakini kama utamwamini Mungu kwa moyo wako wote, unaweza kupata afya. Unaamini hilo? Unaamini? Basi inuka kutoka kitandani mwako. Usiwe na shaka moyoni mwako, usitilie shaka hata kidogo, nenda zako nyumbani, chukua kitanda chako uende nyumbani. Yesu Kristo atakuponya, kama utaamini. Mungu akubariki.

Ilikuwa ni kitu gani?

Una kadi ya maombi hapo? Vema, utakuwa kwenye mstari wa maombi basi.

306 Na wewe je? Je, una kadi ya maombi? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unaamini? Sikujui, lakini wewe ni . . . Kuna shida gani? Umevurugikiwa kabisa, kama fadhaa, matatizo, umeharibikiwa na kila kitu. Hiyo si ni kweli? Na kwa kweli, sasa hivi unajisikia vizuri. Ni Roho Mtakatifu juu yako. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Utanitii mimi kama nabii Wake? Basi simama kutoka kwenye machela hiyo kwa miguu yako, katika Jina la Yesu Kristo, na uende nyumbani, na uwe mzima.

Ngoja, nataka kukuuliza jambo fulani. Huna kadi ya maombi, sivyo? Huihitaji. Wewe ni mzima, unaweza kwenda nyumbani sasa na kushangilia.

307 Ni wangapi wenu mnaoamini kwa moyo wenu wote? Basi, kila mtu anayeamini, simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako. Simama katika Jina la Yesu Kristo na uamini ya kwamba umeponywa. Ninawakabidhi kwa Mungu kwa ajili ya uponyaji wenu katika Jina la Yesu Kristo. Mungu na awajalie. Amina. Vema.

62-0713 Tangu Wakati Huo
Open Bible Standard Church
Spokane, Washington Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org